## CHADEMA YAITWISHA MZIGO POLISI LAWAMA UTEKAJI NCHINI
UKURASA 2

**MLIPUKO** wa kuhara na kutapika watikisa mitaa ya Morogoro
UKURASA 4

**NAPE** aomba radhi kauli ya goli la mkono, adai ni utani



UKURASA 4

**MZEE** aliyetoweka siku tatu, akutwa ameuawa, viungo mwilini havipo
UKURASA 5



**FLICK AMTAKA OLMO BARCELONA SI WILLIAMS**
UKURASA 22


# Nipashe

Alhamisi Julai 18, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0581741

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


**DAWA ZA KULEVYA**

# Orodha ya wauzaji tayari, kazi inaanza

**JANABI** - Muhimbili: Kila siku tunahudumia waraibu 900; dawa katika mabasi sehemu ya biashara...

*Endelea ukurasa 2*





Rais Samia Suluhu Hassan akifurahia jambo na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mkoa wa Rukwa, baada ya kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa shule hiyo katika Kijiji cha Mtindilo, Laela mkoani humo jana. **PICHA: IKULU**

## Samia afunda kupata mabinti wa aina yake siku zijazo
UKURASA 3

**MICHEZO** **UKARABATI KWA MKAPA SASA WAFIKIA ASILIMIA 35** UK 23

**MAONI, KATUNI UK.6**

# Orodha wauzaji iko tayari, kazi inaanza

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI imesema imekamilisha kanzidata ya wauzaji wakubwa wa dawa za kulevya na imeanza uchunguzi wa watu hao, huku Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) ikisema kila siku inapokea waraibu 900 wanaotumia dawa za usaidizi wa kuacha matumizi ya dawa za kulevya 'methadone'.

Hayo yalielezwa jana jijini Dar es Salaam katika mkutano wa waandishi wa habari na Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), Aretas Lyimo, pamoja na Mkurugenzi wa MNH, Prof. Mohamed Janabi.

Pamoja na mambo mengine, mkutano huo ulikuwa na lengo la kutoa taarifa kuhusu kukamatwa kwa wafanyabiashara wanaojihusisha na biashara ya dawa za kulevya.

Prof. Janabi alisema: "Ukubwa wa hili tatizo (matumizi ya dawa za kulevya), ni kubwa sana. Kwenye kanzi data yetu (MNH) hadi Juni, mwaka huu watu 3,840 wanapata tiba ya dawa ya methadone pale Muhimbili."

Alisema kila siku watu 900 wanakuja kunywa tiba ya methadone MNH, kwamba ndiyo kituo chenye watu wengi walioathirika na matumizi ya dawa za kulevya kuliko sehemu yoyote hapa nchini.

Alisema dawa za kulevya zina athari nyingi mojawapo ni kuharibu mfumo wa umeme wa moyo na ndiyo sababu vijana wengi wanapata matatizo na kusababisha vifo vya ghafla.

Pia, zinaharibu figo, akitoa takwimu kwamba MNH inasafisha wagonjwa 150 kwa siku wenye matatizo ya ugonjwa huo, ambao wanahudumiwa kwa vipindi vitatu.

"Kuna sababu kubwa tatu za figo kuharibika, kwanza figo zilizoathiriwa kwa sababu ya shinikizo la damu na kisukari na magonjwa mengine. Pili, matumizi mabaya ya dawa na hizi dawa za kulevya ni sehemu ya tatizo," alisema Prof. Janabi.

Kadhalika, alisema wanaotumia dawa za kulevya wanapata ugonjwa wa saratani kwa sababu wanachangia sindano na kupata homa ya ini, baadhi yao wanaugua saratani ya ini.

**WAFANYABIASHARA KUKAMATWA**

Kamishna Jenerali wa DCEA, Aretas Lyimo, alisema mamlaka hiyo imemkamata mkazi wa Jiji la Dar es Salaam, Shaban Adam (54) kwa tuhuma za kutengeneza dawa za kulevya.

Alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa nyumbani kwake Juni 11, mwaka huu, akitengeneza dawa za kulevya aina ya heroin kwa kutumia dawa tiba zenye asili ya kulevya, akichanganya na kemikali bashirifu.

Pia alisema DCEA inamshikilia, Mbaba Issa ambaye alikamatwa katika Uwanja wa Ndege wa Melchior Ndadaye Bujumbura, Burundi akielekea Dubai akiwa na kilo 3.8 za dawa za kulevya aina ya skanka.

Vilevile, alisema DCEA ilifanya operesheni katika mikoa ya Mwanza, Dodoma, Mtwara na Mbeya na kukamata magunia 285 ya bangi, kilo 350 za dawa za kulevya, milimita 115 za dawa tiba zenye asili ya kulevya pamoja na lita 19,523 za kemikali bashirifu.

Alisema katika operesheni hiyo watuhumiwa 48 wamekamatwa na watafikishwa katika vyombo vya sheria.

**KANZI DATA**

DCEA imekamilisha kanzi data ya wauzaji wakubwa wa dawa za kulevya pamoja na kuanza uchunguzi kuhusu watu hao.

"Wengi wamebainika wapo ndani ya nchi na wengine nje ya nchi. Baadhi yao wana biashara nyingine halali, lakini wanajihusisha na biashara ya dawa za kulevya na kufanya utakatishaji," alisema.

# ACT-Wazalendo kuiburuza Tume Huru mahakamani

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema kiko katika hatua ya mwisho kwa ajili ya kuiburuza mahakamani Tume Huru ya Uchaguzi (INEC), kwa madai haipo kihalali.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Naibu Katibu Mkuu wa Habari, Uenezi na Mawasiliano kwa Umma wa ACT-Wazalendo, Shangwe Ayo, alisema watashirikiana na wadau mbalimbali wapenda demokrasia.

Aidha, wajumbe wote wa zamani wa Tume hawatokani na mabadiliko yaliyofanyika ya sheria za uchaguzi, na kwamba wanatakiwa waondoke ili wateuliwe wengine wapya watakaopatikana kwa mujibu wa matakwa ya sheria mpya za uchaguzi.

"Chama cha ACT-Wazalendo kwa kushirikiana na wengine ambao wanapenda demokrasia, tuna mpango wa kwenda mahakamani kuishtaki INEC ya sasa na hatua ya mwisho ya mipango hiyo ya kuiburuza iko mwishoni, tukiamini kwamba haina mamlaka ya kuwapo pale kwa mujibu wa sheria mpya za uchaguzi," alifafanua Shangwe.

Vilevile, alisema chama hicho kimeanza maandalizi ya kusajili wanachama wake zaidi katika kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu na kwa kuanza wamepanga kusajili wanachama milioni 10 kwa njia ya kidijitali katika ziara iliyopangwa kufanyika katika mikoa 22 kuanza Julai 22, mwaka huu.

Shangwe alisema ziara hiyo itagawanywa katika makundi manne kwa kuongozwa na kiongozi wa chama hicho, Dorothy Semu, kiongozi mstaafu, Zitto Kabwe, Makamu Mwenyekiti Bara, Isihaka Mchijinjita na Katibu Mkuu, Ado Shaibu.

"Kiongozi wa chama atakwenda majimbo 30 ya mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Dodoma, Singida, na Manyara wakati Makamu wake Mchinjita atakwenda katika majimbo 38 ya Ruvuma, mkoa wa kichama Selous, Mtwara, Lindi, Pwani na Tanga.

"Zitto atakwenda katika majimbo 36 kwenye mikoa ya Kigoma, Rukwa, Katavi, Tabora, mkoa wa kichama Kahama na Shinyanga wakati Katibu Mkuu, Shaibu atakwenda katika majimbo 21 ya mikoa ya Mwanza, Simiyu, Mara, Geita na Kagera," alisema Shangwe.

Alisema mpaka sasa wanachama waliosajiliwa na chama hicho kwa mfumo wa kisasa ni milioni moja.

# CHADEMA yaitwisha mzigo polisi lawama utekaji nchini

**Na Joyce Lameck**

SIKU chache baada ya Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP) Camilius Wambura kukanusha madai ya jeshi hilo kuhusika na kuteka watu, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimeendelea kusisitiza kuwa linahusika.

Jana Naibu Katibu Mkuu wa CHADEMA Bara, Benson Kigaila alinyooshea kidole jeshi hilo kuwa linahusika na utekaji mwanachama wao, Kombo Mbwana (29), aliyetekwa Juni 15, mwaka huu.

Kijana huyo alipotea kwa siku 29 mkoani Tanga, huku ndugu zake pamoja na viongozi wa chama hicho wakimtafuta katika vituo mbalimbali vya polisi bila mafanikio.

Pia alimtaka IGP Wambura kujibu maswali aliyoulizwa katika mkutano wa waandishi wa habari mkoani Tanga, ili kuhakikishia Watanzania jeshi hilo halikuhusika na kutekwa kwa kijana huyo.

"Inawezekanaje Jeshi la Polisi kushikilia mtuhumiwa kwa kosa la matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii bila kufikishwa mahakamani ndani ya siku zote hizo? Na toka mwanzo jeshi lilikataa kuwa halijamkamata mtu huyo.

"Baada ya kukataa, siku 29 baadaye ndipo wanakuja kukubali kuwa mtu huyo wanaye kituoni wanamshikilia kwa kosa hilo. Je, ni sheria gani ya Jeshi la Polisi au Sheria ya Tanzania inayosema hivyo?" alihoji.

IGP Wambura, akiwa ziarani mkoani Simiyu hivi karibuni, alisema kazi ya jeshi hilo ni kulinda na kuimarisha usalama wa raia na mali zao na wala si matendo hayo ambayo limekuwa likihusishwa nayo mara kwa mara.

"Lakini jambo hili limekuwa likielezwa na makamanda wa polisi katika maeneo ambayo ripoti hizo zimekuwa zikitolewa. Kwanza, ifahamike kuwa hatuhusiki na shughuli hizo za utekaji watu.

"Sisi ni jeshi linalolinda usalama wa raia na mali zao. Kwa hiyo, wanaoleta tuhuma za namna hiyo kwetu ni vitendo vya kutukosea adabu," alisema IGP Wambura.

Julai 15, mwaka huu, Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Zacharia Benard, alithibitisha kushikiliwa kwa mtu huyo na kueleza kuwa anakabiliwa na tuhuma za matumizi mabaya ya mtandao.

Alisema mtuhumiwa huyo anashikiliwa na jeshi kwa tuhuma za kutumia vibaya mitandao ya kijamii katika mikoa mbalimbali nchini na vifaa vya kielektroniki pamoja na laini za simu za mitandao mbalimbali zisizokuwa na usajili wake katika kutekeleza uhalifu huo kinyume cha sheria za nchi.

Alisema upelelezi wa matukio hayo umefika hatua nzuri na mshtakiwa atafikishwa mahakamani, akitoa wito kwa raia kuacha kujihusisha na matumizi mabaya ya mitandao badala yake kuitumia vizuri kwa manufaa yao na taifa kwa ujumla.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi akikabidhi zawadi ya mlango wa Zanzibar kwa mgeni wake, Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Mashauriano ya Kisiasa la China (CPPCC) kutoka Jimbo la Shandong, Zhang Xinwen, baada ya kumaliza mazungumzo yao Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

**HABARI KITAIFA**

# Samia afunda mabinti kupata aina yake siku zijazo

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan amewataka walimu kulea wanafunzi kwa upendo waje kuwa raia wema, wachapakazi na kutengeneza vizazi vizuri.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wananchi wa maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Rukwa, alipohitimisha ziara ya siku tatu katika mkoa huo na kuweka jiwe la msingi katika Shule ya Wasichana ya Mkoa wa Rukwa, ujenzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya, Kampasi ya Rukwa, ujenzi wa barabara ya lami kwenda Kaengesa Seminari na kuzungumza na wananchi wa Manispaa ya Sumbawanga.

Akiweka jiwe la msingi Shule ya Wasichana Rukwa, Rais alisema walimu wasijikite kwenye kufundisha pekee bali wawalee wanafunzi hao kwa upendo ili waje kuwa mfano mzuri na kutengeneza vizazi vingine vizuri.

Alisema ujenzi wa shule hiyo ni sehemu ya mikakati ya serikali kuweka shule maalum za wasichana za sayansi kila mkoa ili kuwapa uwanda mpana kundi hilo kusomea somo hilo.

Alisema mpango huo umekuja baada ya kuona kuwa wanawake wana uwezo mkubwa wa kujifunza na kumudu masomo hayo, lakini nafasi zilizopo katika shule za kawaida ni finyu.

Aliwasisitiza wanafunzi hao kusoma kwa bidii na kwamba watakaofaulu vyema kidato cha sita wana wanafasi kubwa ya kupata ufadhili wa masomo ya elimu ya juu kupitia mfuko wa 'Samia Schorlaship' ndani na nje ya nchi.

Akiweka jiwe la msingi, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya, Kampasi ya Rukwa, alisema uwapo wa chuo hicho unasogeza huduma ya elimu ya juu na kuongeza mzunguko wa fedha na kuwaongezea maendeleo.

Aliagiza idara ya injinia katika chuo hicho ifundishe vijana wa mkoa huo teknolojia ya kutumia rasilimali ya udongo kutengeneza matofali na vijana wa mkoa huo wafundishwe utaalamu huo.

Akiwa Kaengesa, Rais alisema ujenzi wa barabara hiyo utakamilika mwishoni mwa mwaka huu na kuwasisitiza wananchi wa eneo hilo kuongeza juhudi katika shughuli zao za uzalishaji ili nchi ipate mapato zaidi na kunufaika. Aliwakumbusha wananchi uchaguzi wa serikali za mitaa Novemba, mwaka huu wajitokeze kwa wingi kujisajili kwenye daftari la kudumu la wapiga kura na wakichague Chama cha Mapinduzi (CCM) ili wendelee kuiletea nchi hiyo maendeleo.

Alisema pia wameboresha vifaa vya kupimia nafaka vya Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) na sasa wanatumia mizani ya kieletroniki na simu za kisasa ili kupata uzito halisi na nafaka zinazouzwa na mkulima na kuondoa malalamiko.



Alimwagiza Waziri wa Kilimo, Husein Bashe kuongeza bei ya kununua mahindi kutoka kwa wakulima kufikia Sh. 700 kwa kilo ili wapate faida itakayowaridhisha.

Katika msimu ujao wa kilimo, alisema mbegu za mahindi zitolewe kwa ruzuku ili kuwapunguzia mzigo wakulima na kuwapa motisha wa kuendelea kulima na kuongeza mazao.

Alisema uamuzi wa serikali kulifungua Ziwa Victoria ulifanywa kwa nia njema ya kuongeza uzalishaji wa samaki ili likifunguliwa wavuvi wapate bidhaa za kutosha.

Aliwasisitiza wananchi wajitokeze kutoa maoni yao kuhusu aina ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2050 ili itakapotoka iwe imekidhi mahitaji ya Watanzania wote.

Waziri wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), MohamedMchengerwa, alisema ujenzi wa shule hiyo maalum kwa wanafunzi wenye vipaji ni sehemu ya maagizo yake ya kujenga shule moja ya sayansi kwa wasichana katika kila mkoa na mpaka sasa mikoa 25 imeshakamilisha ujenzi na watoto wameshaanza masomo na kutumia jumla ya Sh. bilioni 104 kati ya 106 zilizotengwa.

Alisema katika mradi wa shule hiyo ya mkoani Rukwa Sh. bilioni 23 zimekwisha tolewa na nyingine zitatumwa hivi karibuni, majengo 19 kati ya 23 yamekamilika, manne ikiwamo bwalo la kulia chakula ujenzi unaendelea.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alisema ujenzi wa chuo hicho utasaidia kutolewa shahada ya kwanza teknolojia ya kilimo kwa ajili ya kuendeleza sekta ya kilimo ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa elimu ya juu kwa mageuzi ya uchumi.

Alisema chuo hicho kimejikita kwenye kilimo kwa kuwa ndio shughuli kubwa ya kiuchumi ambayo mkoa huo unajielekeza, hivyo kitasaidia kuongeza uzalishaji wa mazao na kukuza uchumi wa watu wa eneo hilo na Watanzania kwa ujumla.

Kuhusu barabara Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara (TANROAD), Mohamed Besta, alisema kuwa itajengwa kwa kiwango cha lami na mpaka sasa imekamilika kwa km 1.4 kati ya sita inayotarajiwa na kugharimu, Sh. bilioni 6.2.


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya **epaper.ippmedia.com** utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza **"subscribe"**
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa **kadi ya benki** malipo kwa **mtandao wa simu** unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa **namba ya simu** unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. **Kwa benki** unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya **www.ippmedia.com** upande wa kulia utaona **"E-Paper"** utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

## GOLI LA MKONO

# Nape aomba radhi, adai ulikuwa utani

**Na Halfani Chusi**

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye ameomba radhi wananchi na wapenda demokrasia kufuatia kauli yake aliyodai ya utani aliyoitoa akiwa katika Jimbo la Bukoba Mjini juzi.

Akiwa jimboni huko, Nape alisikika akisema: "Unajua nyie sikilizeni, matokeo ya kura si lazima yawe ya kwenye boksi, inategemea nani anahesabu na kutangaza.

"Na kuna mbinu nyingi; kuna halali, nusu halali na kuna haramu na zote zinaweza kutumika mradi tu mkishamaliza unamwambia Mwenyezi Mungu nisamehe pale nilipokosea."

Kauli hiyo ilizua mjadala katika mitandao ya kijamii, wadau wa demokrasia nchini wakiitafsiri ina nia ya kutonesha tena kidonda uchaguzi uliopita.

Chama anakotoka Mbunge huyo wa Mtama, Chama Cha Mapinduzi (CCM), hakiko mbali na kauli hiyo, juzi kikatatoa kauli kwamba alichokisema Nape ni mtazamo wake, si kauli ya chama chao.

Waziri Nape ambaye pia aliwahi kuwa Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM - Itikadi na Uenezi, jana aliomba radhi huku akisisitiza ulikuwa ni mwendelezo wa utani wa jambo la goli la mkono lililojitokeza miaka tisa iliyopita na amekuwa akitaniwa nalo.

Alisema ameona mjadala unaozungumzia utani alioufanya Bukoba, na kwamba utani huo umedumu kwa muda mrefu, lakini kwa kipindi hiki umekuwa mjadala mrefu kwa sababu nchi iko katika mchakato wa uchaguzi.

"Niseme kama kiongozi, mtu mzima ninadhani ninawajibika kuwapa pole na kuwaomba radhi wale ambao wamesumbuliwa na kuteswa na huu mjadala.

"Ninasisitiza kwamba ulikuwa utani, ambao haukuwa na ukweli ndani yake, haukuwa na jambo 'serious' (makini) na mimi nimeukubali utani huo tangu wakati huo niliutolea ufafanuzi wakati ule, lakini vijana wakasema ahh... wewe mzee wa goli la mkono tu na mimi nikaendelea nao.

"Msingi wake ulikuwa ni huo. Kwahiyo, nichukue nafasi hii kusisitiza mimi ni muunimi wa uchaguzi huru na haki na nimuumini wa kuwapa fursa wapigakura waamue kiongozi wanayemtaka na hili nimekuwa ninalifanya kwa miaka yote iliyopita.

"Ninasisitiza kwamba ulikuwa ni utani ambao umekwenda kwa miaka tisa na sijapata nao tabu. Sasa kama kuna mtu amekwazika, ni vizuri nimpe pole na nimwombe radhi, lakini kwa msingi hata tukio lilivyokuwa na nilivyokuwa ninaongea utagundua nilikuwa ninatania," alisema.

Nape alitoa kauli hiyo juzi katika Soko la Kashai alipoalikwa na Mbunge wa Bukoba Mjini, Stephen Byabato kushuhudia ramani na michoro ya soko jipya linalotarajiwa kujengwa.

Katibu wa NEC - Itikadi, Uenezi na Mafunzo CCM, Amos Makalla alifafanua kuhusu kauli iliyotolewa na Nape kwamba si ya CCM.

Makalla alikana kauli hiyo katika mkutano wa hadhara uliofanyika viwanja vya Pangas, Kata ya Wazo, Jimbo la Kawe, Wilaya ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam, wakati wa ziara yake.

Alisema amesikia mitandaoni kuna kiongozi anasema ushindi wa uchaguzi hautokani na kura katika sanduku. Kauli isitazamwe kuwa inatokana na CCM.

Alisema kauli hiyo si msimamo wa chama hicho na CCM inaheshimu demokrasia na kuamini vyama vyote vitashindwa na CCM itashinda kwa haki na itaheshimu uamuzi wowote; aliyeshinda ndiye atakayetangazwa," alisema Makalla huku akisistiza CCM inaamini tume huru ya uchaguzi na msingi ya utawala bora.

Mbali na CCM, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na ACT Wazalendo vililaani vikali kauli ya Nape, vikisisitiza inakinzana na falsafa ya R4 za Rais Samia Suluhu Hassan.

Vyama hivyo kupitia Mkurugenzi wa Mawasilinao, Uenezi na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema na Naibu Mwenezi wa Chama cha ACT- Wazalendo, Shangwe Ayo, pia vilisema kauli ya Nape pia inakiuka misingi ya demokrasia kwamba haina nia njema, ikizingatia uchaguzi unakaribia.

# Mlipuko wa kuhara, kutapika watikisa Manispaa Morogoro

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

UGONJWA wa kutapika, kuhara na kuishiwa nguvu, unaodhaniwa kipindupindu, umelipuka katika maeneo mbalimbali ya Manispaa ya Morogoro na kusababisha Kituo cha Afya Sabasaba kinachotumika kama hospitali ya manispaa kuzidiwa wagonjwa wa aina hiyo.

Hali hiyo imesababisha wagonjwa wanaopokewa kituoni huko kulazimika kupata huduma wakiwa wamelazwa kwenye mabenchi ya kupumzikia wagonjwa, karo la maji, ndani ya vyumba vya madaktari na wengine kulazimika kuwekewa magodoro chini katika kituo hicho ambacho hakina uwezo mkubwa wa kulaza wagonjwa.

Vilevile, baadhi ya watoa huduma wamekuwa wakilazimika kutumia muda zaidi wa saa za kazi kuendelea kubaki kituoni huko kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa wanafikishwa hospitalini huko.

Mwandishi wa habari hii baada ya kupata taarifa za changamoto hiyo, alilazimika kuungana na watu wengine watano kwenda katika kituo hicho cha afya mnamo Julai 16 mwaka huu, saa tano usiku na kukuta hali ni mbaya kwa wagonjwa kulazwa maeneo mbalimbali yasiyo rasmi ikiwamo kwenye mabenchi, chumba cha daktari, sakafuni na kwenye karo.

Hadi majira hayo, tayari kulikuwa na wagonjwa 11 na hadi wanaondoka eneo la tukio, saa saba usiku, wagonjwa walishafikia 12, wakidaiwa kutokea maeneo ya Kihonda Yespa, kulikokuwa na mkutano wa Injili wa Nabii Joshua pamoja na maeneo mengine ya mji na siku iliyofuata, hadi mchana kituo hicho kilikuwa kimeshapokea wagonjwa 14.

"Kama hujazidiwa sana ninashauri uondoke, ukapate matibabu nyumbani, hapa unaona hatuna hata kitanda, wote hawa ni kipindupindu, wanaharisha na kutapika, lakini vinginevyo sijui, bora wewe una nguvu, hawa hawajiwezi kabisa," mmoja wa watoahuduma alimwambia mwandishi aliyedai kusumbuliwa na changamoto ya kuhara.

Baada ya kupewa taarifa hizo, mwandishi aliamua kuondoka kituoni huko pamoja na timu yake ya watu watano waliokwenda kuchunguza kinachoendelea, wakiacha wagonjwa wakiwa wamelazwa maeneo mbalimbali kituoni huko.

Kabla ya kuondoka kituoni huko, Mganga wa Zamu aliyejitambulisha kuwa ni Dk. Facilius Zanzibar na alipoelezwa kuwa aliyefuata huduma ni mwandishi wa habari, alikiri kuingia zamu tangu saa nane mchana na alitarajia kutoka saa mbili usiku, lakini hadi saa tano usiku alikuwa anaendelea na huduma kutokana na idadi kubwa ya wagonjwa.

Dk. Zanzibar alisema kituo hicho cha Sabasaba kimekuwa kinapokea wagonjwa wa kuharisha "maji meupe" na kutapika mfululizo na walishapima awali wenye dalili za aina hiyo hiyo kwa wagonjwa wa Januari iliponyesha mvua na kugundua ni ugonjwa wa kipindupindu.

"Nimemwona huyu yuko stable, nimemshauri apate ORS, apate na Dox (Doxycycline ) na aende akajiuguze nyumbani, ila huko azingatie ORS," alisema daktari wa kike akimweleza mganga wa zamu kuhusu changamoto ya mwandishi.

Dk. Zanzibar aliulizwa kinachojiri, athibitisha hali ni mbaya kituoni, walikuwa na wagonjwa watano, lakini wengine waliendelea kupokewa kufikia 11 kufikia saa mbili usiku siku hiyo, wakiwa na dalili za kuharisha na kutapika. Kati yao, watatu walikuwa wa familia moja kutoka Lukobe, wengine watatu kutoka Kihonda Yespa kulikokuwa na mkutano wa mahubiri, wakijumuisha mama na watoto, na wengine.

Alisema wagonjwa wamekuwa wakipungua na kuongezeka kutoka maeneo mbalimbali ya Morogoro wakiwa na dalili hizo za kutapika na kuhara.

Alitaja maeneo mengine wanakotoka wagonjwa hao ni pamoja na Kasanga, Kata ya Mindu, Mji Mwema, Tubuyu, Kichangani, Msamvu Ndege Wengi, Vibandani na Mazimbu (Dark City), hivyo kuhimiza elimu zaidi kuendelea kutolewa kwa wananchi Ili kupunguza au kumaliza tatizo hilo vinginevyo ugonjwa utazidi kuenea.

Kuhusu wagonjwa waliolazwa, alisema hawezi kusema hali zao ni nzuri au mbaya, lakini hawako vizuri na wanaendelea na matibabu na kukiri wagonjwa kulazwa maeneo mbalimbali kutokana na kukosa maeneo ya kutosha kutokana na dharura ya ugonjwa wenyewe.

"Tuna vyumba viwili tu kwa ajili ya kupumzisha wagonjwa na chumba cha sindano tuna kitanda kimoja na pia tuna magodoro mawili ya dharura, ndio maana hapa godoro moja tumewaweka watoto watatu kwa pamoja hapo chini," alisema Dk. Zanzibar.

Alipoulizwa "sababu za kutopeleka wagonjwa hao kambi maalum iliyokuwa imetengwa miaka ya nyuma maeneo ya Sabasaba na Mazimbu, daktari huyo alisema kituo cha afya ambacho hakijaanza kazi cha Mazimbu kiko mbioni kufungwa na uongozi kutokana na kukosa wagonjwa.

Wakati mazungumzo na daktari huyo yakiendela, saa sita usiku aliingia Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Sabasaba, Dk. Henry Mungia na kuanza kuwafokea waandishi wa habari, akiwahoji aliyewapa kibali cha kupiga picha kituoni huko.

Alipoelezwa kuwa waandishi walikuwa sehemu ya wagonjwa, aliwataka waende naye ofisini kwake. Huko Dk. Mungia alizungumza nao kwa masharti ya kutorekodiwa hadi idhini ya bosi wake ikitoka. Alikwenda nje kuzungumza kwa simu, akitumia muda mrefu, na alipofuatwa nje na kurudi ofisini kwake, aliingia Mganga Mkuu wa Manispaa ya Morogoro, Dk. Focus Maneno naye aliingia ofisini.

Dk. Maneno alizungumza na waandishi kwa masharti ya kutorekodiwa kisha akaagiza waandishi wa habari waondoke, waache watoahuduma waendelee kutibu wagonjwa.

Waandishi walikubali kuondoka kwa makubaliano kwamba siku iliyokuwa inafata, yaani jana, saa tatu asubuhi wangekutana na Mganga Mkuu wa Manispaa kuzungumzia tukio hilo.

Hata hivyo, wakati wanaandishi wakijiandaa kuondoka kituoni huko, gari la wagonjwa lilifika saa saba usiku na kuanza kuwahamisha wagonjwa kuwapeleka kambi maalum ya kipindupindu iliyoko Mazimbu.

Mganga Mkuu wa Manispaa ya Morogoro, Dk. Focus Maneno alipofuatwa jana asubuhi kuzungumza hali ya kipindupindu na hatua wanazochukua kukabiliana na ugonjwa huo, alikataa kutoa maelezo yoyote kwa kuwa "timu yake ya wataalamu iko mitaani kufanya tathmini kwanza".

Pia aliwataka waandishi wa habari waanzie kwa Ofisa Habari wa Manispaa ili naye ampe mwongozo wa kuzungumza nao kwa kuwa ndio mwongozo wa manispaa hiyo kiutendaji.

Hata hivyo, alisisitiza kuwa siyo kila anayeharisha na kutapika ni mgonjwa wa kipindupindu.

Waandishi walimtafuta Ofisa Habari wa Manispaa, Lilian Henrico ambaye hakuwa ofisini na alipopigiwa simu, alishikilia msimamo wa Dk. Maneno kuwa watatoa taarifa baada ya tathmini kukamilika.

Hata hivyo, Mganga Mkuu wa Manispaa na Ofisa Habari huyo hawakutaka kuweka wazi lini tathmini ingemalizika na kutolewa taarifa.

Baadhi ya wakazi wa Manispaa ya Morogoro, wakiwamo Monica Malya, mkazi wa Kata ya Mindu; Joyce Mihambo, mkazi wa Kata ya Kichangani; Erica Francis wa Kihonda Yespa na Mussa Abubakary wa Wilaya ya Morogoro, kwa nyakati tofauti walisema hawajasikia taarifa za kuwapo mlipuko wa kipindupindu wala wagonjwa wa kuhara na kutapika katika maeneo yao, lakini wakaomba kama magonjwa hayo yapo ni vyema jamii ikapewa elimu.

"Wananchi waelimishwe kuchukua tahadhari wakati wote kwa kuhakikisha wananawa mikono kabla na baada ya kulaz kufunika vyakula,kula vyakula vya moto na kuacha kula kula ovyo, wahimizwe pia kuwahi hospitalini kupata tiba, Ninazijua dalili za kipindupindu ni kuharisha wakati wote maji meupe na kutapika lakini siyo wote wanajua," alisema Joyce Mihambo.

Mussa Abbubakar, mkazi wa Morogoro, alisema ni vyema maofisa afya wakapita kwa wananchi kutoa elimu mitaani kwa kutumia magari ya matagazo na vyombo vya habari kuelimisha watu kuhusu ugonjwa huo na kupiga marufuku ulaji katika mikusanyiko na zaidi elimu ifikishwe vijijini.

Januari mwaka huu katika Baraza la Madiwani Manispaa ya Morogoro liliagiza madiwani na watendaji wa kata na mitaa kuhakikisha wanaendelea kuelimisha wananchi kuhusu ugonjwa wa kipindupindu, hasa elimu ya kujikinga na maambukizi.

## Makalla atoa angalizo mradi Stendi Mpya Mabasi Mwenge

**Na Romana Mallya**

KATIBU wa NEC, Itikadi, Uenezi na Mafunzo CCM Taifa, Amos Makalla, ameagiza mradi wa Stendi Mpya ya Mabasi Mwenge, Manispaa ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam uwe shirikishi ili kuondoa migogoro.

Makalla alitoa agizo hilo jana baada ya kutembelea mradi huo ikiwa ni ziara yake ndani ya mkoa huo kuona miradi inayotekelezwa.

Akizungumza na wananchi waliokusanyika kituoni hapo, Makalla alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuukwamua mradi huo baada ya kusimama kupisha uchunguzi wa tume iliyoundwa hapo awali.

"Lengo la mradi huu ni kuchochea biashara, inawezekana kukawa na changamoto mbalimbali za kutoelewana, lakini wote tulitamani maduka hapa.

"Kila mmoja alitamani awe sehemu ya mradi, niwaombe mwendelee kutoa elimu, lakini pia ukawe shirikishi kwa makundi mbalimbali yanayotoa huduma katika stendi hii.

"Sio iwe kuanzia leo fulani na fulani...hapana mkae muone yale mliyoyapata na makundi mengine yashirikishwe ili mfurahie," aliagiza Makalla.

Mchumi wa Manispaa ya Kinondoni, Jabir Chilumba, alisema hadi kukamilika mradi huo unatarajia kutumia Sh. bilioni 12.283 kwa mapato ya ndani ya halmashauri ikiwa ni gharama ya utekelezaji wa mradi kwa kipindi cha Force Account ' ilikuwa ni Sh. bilioni 2.216.

Alisema gharama za ujenzi kipindi cha kandarasi ilikuwa ni Sh. bilioni 10.067.

Alisema jengo hilo lina jumla ya sakafu tatu zenye fremu 148 ambazo zinaweza kutumika kwa matumizi mbalimbali ya kibiashara.

"Matarajio ya halmashauri ni kukusanya Sh. bilioni 1.093 kwa mwaka ambapo mwekezaji anatakiwa kulipa Sh. milioni 612.744 na wapangaji wa fremu zilizobaki wanapaswa kulipa Sh. milioni 480.623.

Alisema makusanyo hadi mwezi Juni, 2024 ni Sh. bilioni 1.039, mwekezaji amelipa Sh. milioni 612.744 na wapangaji katika mnada mtandao wamelipa Sh. milioni 426.397.

# Mzee aliyechukuliwa na watu wasiojulikana auawa kikatili

## ●Baadhi ya viungo vyake vyanyofolewa

**Na Moses Ng'wat,** MBOZI

KUMINYA Sambo (63), mkazi wa Kijiji cha Nambizo, wilayani Mbozi, mkoani Songwe, amekutwa akiwa ameshafariki dunia, akidaiwa kuuawa na watu wasiojulikana kisha mwili wake kutupwa msituni kijijini huko.

Taarifa zilizothibitishwa na ndugu pamoja na uongozi wa kijiji zinadai kuwa mzee huyo ambaye hakuwa na mke, alitoweka nyumbani kwake siku kadhaa kabla ya kukutwa akiwa ameuawa, huku viungo vya mwili wake ikiwamo mguu na mkono vikiwa vimenyofolewa.

Mmoja wa watoto wa marehemu aliyejitambulisha kwa jina la Jose Kuminya, alisema baba yao alikutwa ameuawa baada ya kutoonekana kwa siku tatu.

Jose alisema Mzee Sambo alipotoweka nyumbani usiku wa Julai 9 mwaka huu, walianza kumtafuta kwa kushirikiana na wananchi hadi siku ya tatu Julai 11, mwaka huu walipokuta mwili wake umetelekezwa kando ya njia katika msitu kijijini huko, huku mguu mmoja na mkono vikiwa vimenyofolewa.

Alisema kuwa mazingira yaliyokutwa nyumbani kwa baba yao ambaye alikuwa akiishi peke yake, siku aliyotoweka yalizua hofu kubwa kwa kuwa walikuta hakuna dalili zilizoonyesha kama nyumba ilivunjwa.

"Mlango haukuvunjwa, hali inayoonesha watu waliomchukua baba na kwenda kumuua, waliondoka naye baada ya kumgongea na yeye kuwafungulia mlango kwani hata pombe aliyokuwa akitumia usiku ule ilikutwa kwenye kopo ikiwa pembeni," alidai Jose aliyesimulia tukio hilo kwa hisia kali.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Namanga kijijini huko, Jackson Ntembo, alithibitisha kutokea tukio hilo na kusema kuwa baada ya kupewa taarifa za kutoweka kwa Mzee Sambo, walianza msako, hatimaye kumkuta akiwa amefariki huku akiwa amekatwa kwa kitu chenye ncha kali kifuani na kichwani huku mguu mmoja na mkono vikiwa vimenyofolewa.

"Daktari aliufanyia uchunguzi mwili wa marehemu na kukuta una majeraha manne ambayo yalisababishwa na kukatwa na kitu chenye ncha kali, na mimi kama kiongozi, ninaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi zaidi kuhusu tukio hilo," alisema Ntembo.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Gallus Hyera, alithibitisha kutokea tukio hilo na wanaendelea na uchunguzi. Hadi jana, hakuna mtu aliyekuwa amekamatwa kuhusiana na tukio hilo.

Wilaya ya Mbozi imekuwa na matukio ya mauaji. Hivi karibuni, watu wasiojulikana walimuua aliyekuwa Mfamasia wa Kituo cha Afya cha Isansa, wilayani hapa, Daudi Kwibuja (30) na mwili wake kukutwa kando ya barabara kuu ya Mbeya-Tunduma (Tanzam) katika eneo la Mlowo.

Mwili wa mtumishi huyo ulikutwa ukiwa na majeraha. Taarifa ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Agostino Senga, ilibainisha kuwa uchunguzi ulionesha majeraha katika mwili wa marehemu hayakuwa ya ajali ya kugongwa na gari. Awali ilidhaniwa kuwa mfamasia huyo alifariki dunia kwa ajali ya gari.

Kama ilivyo kwa tukio la Mzee Sambo kuuawa na kunyofolewa viungo, hadi jana hakuna mtuhumiwa aliyekuwa amekamatwa na Jeshi la Polisi dhidi ya mauaji ya mfamasia huyo.




Naibu Katibu wa Habari, Uenezi na Mawasiliano kwa Umma wa Chama cha ACT Wazalendo, Shangwe Ayo, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu ziara ya viongozi wa chama hicho ya kwenda mikoa 22 itakayoanza Julai 22, mwaka huu, yenye lengo la kusajili wanachama wapya milioni 10. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wanafunzi wote kaya masikini kupata mkopo elimu ya juu kwa asilimia 100

**Na Restuta James,** ARUSHA

MFUKO wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) umeweka mazingira ya kuwezesha wanafunzi wote wanaojiunga na elimu ya juu kutoka kaya maskini, kupata mkopo kwa asilimia 100 ili watimize ndoto zao.

Katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2021/22, wanafunzi 4,600 wamenufaika kutokana na TASAF kuwatambulisha kwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB).

Hayo yalielezwa jana jijini hapa na Mkurugenzi wa Mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) wa TASAF, Justine Boaz, alipozungumza na waandishi wa habari waliotembelea wanufaika wa mfuko huo katika wilaya za Arusha na Moshi.

Alisema wanafunzi kutoka kaya zinazoishi katika umaskini uliokithiri, wanapata mkopo kwa asilimia 100 kwa kozi yoyote chuo kikuu.

"Na kwa sasa tumeongea na HESLB ili watoto wanaotoka kaya maskini wapate mikopo mara tu chuo kinapofunguliwa badala ya kusubiri wiki mbili au tatu. Nia ni kuwezesha kufika chuo kwa wakati na kuwaepushia usumbufu.

"Tupo katika hatua za mwisho kuhakikisha hili linafanikiwa na tayari mifumo yetu inasomana na bodi. Mwanzoni tulikuwa tunawapa barua ya utambulisho lakini sasa hivi tunataka wakishathibitishwa tu chuoni, bodi inawasoma na kuwapatia mkopo," alisema mkurugenzi huyo.

Mmoja wa wanufaika wa TASAF, Caroline Minja wa Mtaa wa Kariwa Chini, Kata ya Rau, Manispaa ya Moshi, alisema mtoto wake ni miongoni mwa wanufaika wa mfumo huo na sasa anasoma Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka.

Takwimu za serikali zinaonesha asilimia nane ya Watanzania wanaishi katika lindi la umaskini, wakishindwa kumudu milo mitatu kwa siku.

Dhima kuu ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 ni kupunguza walau nusu ya wananchi wanaoishi katika umaskini na kuwafanya waishi katika uchumi wa kati ifikapo 2025, yaani mwakani.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kodi ndio msingi wa maendeleo, lazima ilipwe

**NCHI** yoyote duniani iliyoendelea, maendeleo yake yanatokana na kodi zinazokusanywa na serikali za nchi hizo kupitia vyanzo mbalimbali vya mapato.

Kodi hizo ndizo zinazofanikisha miradi ya ujenzi ya barabara, vituo vya afya, shule na ununuzi wa bidhaa muhimu zikiwamo dawa za kutibu magonjwa makubwa.

Ukusanyaji wa kodi unatakiwa uonekane utekelezaji wake kwa vitendo kwa kufanikisha miradi ambayo watu wataridhika nayo kulingana na kodi wanazolipa.

Mara nyingi malalamiko hujitokeza wananchi wanapoona wanakatwa kodi, lakini fedha zinaelekezwa kwenye matumizi mengine ambayo hayawagusi moja kwa moja.

Vyanzo vya makusanyo ya kodi viko vingi na kama kila mwananchi angewajibika kuilipa nchi yetu ingekuwa mbali kimaendeleo.

Kwa nchi ambazo zimepiga hatua katika maendeleo, mengi yametokana na kodi zinazokusanywa na serikali.

Wananchi pia wanaelewa umuhimu wa kulipa kodi kwasababu wanaona faida zake katika kuwahudumia kwenye sekta mbalimbali.

Udanganyifu katika ulipaji kodi unarudisha maendeleo na kuifanya serikali kubeba mzigo mkubwa kutekeleza baadhi ya miradi kwa kutegemea ufadhili au mikopo kutoka kwenye nchi zilizoendelea.

Baadhi ya wafanyabiashara hudiriki kufanya udanganyifu kwenye ulipaji kodi kwa kuandika risiti zisizo za uhalisia na bidhaa walizomuuzia mteja.

Uaminifu kwa pande zote za ulipaji na ukusanyaji ni jambo muhimu sana ili kufikia hatua zilizofikiwa na nchi nyingine duniani zilizoendelea.

Wakati mwingine uaminifu unakosekana kutokana na walipakodi kuona fedha zao zinatumika vibaya kinyume na makusudio.

Rais Samia Suluhu Hassan, amekuwa akihamasisha wananchi kulipa kodi ili nchi iweze kusonga mbele na kukamilisha miradi ambayo imekwama kwa kukosa fedha.

Amekuwa akisisitiza kuwa ili nchi itekeleze miradi ya maendeleo wananchi hawana budi kulipa kodi zinazowekwa na serikali haijalishi ni ndogo au kubwa ili mradi iwe halali.

Tozo ndogo ndogo pia husaidia kwenye mapato na
kujenga barabara, madaraja, shule na mambo mengine,
kwa sababu hakuna serikali inayoendeshwa kwa pesa nyingine zozote isipokuwa pesa za kodi za wananchi wake.

Hata hivyo, miradi hiyo pia itunzwe ili iweze kudumu na kunufaisha vizazi vijavyo.

Lakini, kuna baadhi ya wananchi hudiriki kuharibu miradi hiyo kwa makusudi na kusababisha hasara ya kuitengeneza tena badala ya kujenga miradi mingine.

Kuna ambao wana tabia ya kuchimba na kulima pembezoni mwa barabara na kusababisha mmomonyoko wa udongo na kuharibu miundombinu hiyo.

Kilomita moja tu ya barabara ni sawa na kujenga vituo vitatu vya afya vya kata pamoja na kuweka vifaa tiba ndani.


Kuna baadhi ya wanaohujumu miradi hiyo kwa kung'oa vyuma vya kingo vilizowekwa kwenye madaraja na kwenda kutengeneza vifaa mbalimbali.

Ukiangalia gharama iliyotumika kutengeneza kingo hizo na vifaa vinavyotengenezwa ni hasara kubwa. Wananchi hawafahamu sio serikali pekee inayoathirika bali hata wewe ambaye unalipa kodi.

Mara ngapi wananchi wanalalamika tozo zinazokatwa kwenye miamala ya simu, kama miundombinu itaendelea kuharibiwa hakuna shaka kuwa unafuu wa tozo hautakuwapo.

Ni muhimu kila mwananchi kuona uchungu na kuwa mlinzi wa mwenzake ili miradi inayojengwa iendelee kudumu na mingine ijengwe kwa lengo la kuleta maendeleo makubwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Mwaka 2024 unagawanyika kwa mbili, tuwaepushe mabinti dhidi ya ukeketaji

**KILA** mwaka unaogawanyika kwa mbili, unatajwa kuwa ni wa mavuno kwa mangariba, wazee wa mila na hata kwa wazazi na walezi ambao wanadumisha mila za ukeketaji, ambazo kimsingi za ukatili wa kijinsia.

Miaka yote, mangariba huwa wanakeketa, lakini mwaka unaogawanyika kwa mbili, unatajwa kuwa unatumiwa na wakeketaji wengi, kutokana na kile kinachoelezwa huwa ni wa baraka na si wa mkosi kama mingine.

Mwaka 2024 unagawanyika kwa mbili, hivyo kutokana na mila za wakeketaji, ni wa baraka na mafanikio, hivyo. inawezekana mabinti na watoto wachanga wakakeketwa kwa wingi.

Desemba ni mwezi ambao hutumika sana kufanikisha vitendo hivyo vya ukatili katika mikoa mbalimbali yenye mila hizo, na hata baadhi ya maeneo ya jiji la Dar es Salaam.

Baadhi ya maeneo hayo, katika jiji la Dar es Salaam yanatajwa kuwa ni Kitunda, Kipunguni na vitongoji vya maeneo hayo. Hivyo ni vyema jamii ikatafakari na kuchukua hatua za kunusuru walio kwenye hatari hiyo.

Kwa kuwa mangariba, wazee wa mila, wazazi na walezi husubiri wakati wa likizo na kufanya vitendo hivyo, ninadhani ipo haja kuwazuia wasichana kwenda likizo ili kuepuka kufanyiwa ukatili huo.

Ni kweli kwamba mapambano dhidi ya ukeketaji yapo, lakini bado vitendo hivyo vinaendelea bila kujali kwamba unasababisha madhara makubwa katika afya ya wasichana na watoto wa kike.

Miongoni mwa madhara yake ni kupoteza uhai, kuvuja damu nyingi pamoja na kupata maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Hivyo ni vyema kila mmoja wetu akahusika katika vita hii.

Si vibaya elimu ikaendelea kutolewa zaidi kuhusu suala hili la mila na desturi kandamizi zilizopitwa na wakati ambazo zinasababisha vitendo hivyo viendelee kutokea ndani ya jamii.

Jukumu la kutoa elimu lisiwe la Wizara ya Afya tu, bali wadau wote wa kupinga ukatili waendelee kuelimisha umma kuhusu madhara makubwa yanayowapata wanawake waliokeketwa.

Lakini, katika suala la kutoa elimu kuhusiana na madhara ya ukeketaji, ni vyema kuwashirikisha wanaume katika michakato mzima wa kupinga ukeketaji nchini, ili nao watoe mchango wao.

Utoaji wa elimu ni wa muhimu, kwani kuna sababu mbalimbali ambazo huwa zinatajwa kuchangia ukeketaji, ikiwamo wanajamii au wanafamilia kuamini kuwa ili mtoto wa kike aweze kuvuka kutoka katika hatua ya kuwa msichana mdogo kwenda kwenye hatua ya kuwa mtu mzima au mwanamke kamili ni lazima akeketwe.

Imani hiyo inaweza kuchangia kuwapo hata kwa ndoa za utotoni, kwani msichana akishakeketwa, wanaume huanza kupeleka posa katika familia husika wakiamini kuwa tayari katika familia hiyo, kuna binti aliye tayari kuolewa.

Lakini ikumbukwe kuwa katika mazingira hayo ya ndoa za utotoni, watoto wa kike wanaweza kukosa fursa au haki ya msingi ya kupata elimu na pia kukosa uhuru wa kufurahia haki nyingine za watoto.

Elimu ni moja kati ya haki muhimu inayopaswa kupata, lakini baadhi ya watoto wa kike hunyimwa baada ya kukeketwa, kwani mara nyingi hulazimishwa kuolewa baada ya kukeketwa.

Wakati huu ambao tuko katikati ya mwaka 2024, ni vyema kukumbuka kuwa unawanyima kwa mbili na ndio ambao wakeketaji huutumia kutimiza vitendo vya ukatili huo kwa mabinti na watoto.

Ni vyema wahusika waendelee kuelimishwa, lakini pia si vibaya jamii kutoa taarifa kwa vyombo vya dola kila inapoona viashiria vya kuwapo kwa vitendo hivyo, ili kunusuru kundi hilo.

Tanzania bila ukeketaji inawezekana, iwapo kila mmoja kwa nafasi yake atashiriki katika vita hiyo, iwe ni kwa kutoa elimu, kutoa taarifa za matukio ya vitendo hivyo au kwa namna yoyote ile.

HABARI KITAIFA

# Waomba jimbo ligawanywe kurahisisha huduma

**Na Gideon Mwakanosya,** NAMTUMBO

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma, Juma Pandu, ameiomba serikali kuligawa Jimbo la Namtumbo ili kurahisisha upatikanaji huduma kwa wananchi.

Kwa sasa jimbo hilo lina kata 21 ambalo kijografia zimekaa mbali na makao makuu ya halmashauri hiyo, likipakana na Wilaya ya Tunduru, Mkoa wa Morogoro na nchi ya Msumbiji.

Pandu ambaye ni Diwani wa Kata ya Mkongo Nakawale, alisema hali ya wananchi wanaohitaji huduma katika halmashauri hiyo wanapata usumbufu mkubwa kufika makao makuu ya halmashauri.

Alisema kwa wakazi wa maeneo ya Kata ya Magazini na Lusewa ambazo zipo umbali wa kilomita zaidi ya 280 hadi makao makuu ya wilaya wanashindwa kusafiri au kutekeleza baadhi ya miradi ya maendeleo kwenye kata zao kwasababu ya umbali, ubovu wa miundombinu hasa wakati wa mvua.

Alifafanua kutoka makao makuu ya wilaya hadi Kata ya Kitanda ni umbali wa kilomita 150, jambo linalosababisha wananchi kukosa baadhi ya huduma za msingi.

"Zipo jitihada zimefanywa za kuiomba serikali ione umuhimu wa kuligawa jimbo ambalo ni kubwa sana, nina imani serikali itaweza kusikiliza kilio cha wananchi wa Jimbo la Namtumbo ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakiomba jimbo hilo ligaiwe," alisema Pandu.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Namtumbo, Zuberi Lihui akizungumza na waandishi wa habari katika Kijiji cha Mputa, alisema Jimbo la Namtumbo ni kubwa na kwamba itakuwa vyema likigawanywa.

Alisema ukubwa wa jimbo hilo ni sawa na Mkoa wa Mtwara ambako kuna majimbo mengi, tofauti lilivyo Jimbo la Namtumbo ambalo linaendelea kuwahudumia wananchi katika mazingira magumu.

Lihui alisema endapo serikali itakubali kuligawa jimbo hilo, Wilaya ya Namtumbo itakuwa na maendeleo zaidi kwa sababu wananchi watakuwa wanapata huduma kirahisi tofauti na ilivyo sasa.

Mbunge wa Jimbo la Namtumbo (CCM), Vita Kawawa, alipohojiwa na waandishi wa habari kuhusu ombi hilo, alisema ni kweli jimbo ni kubwa na anapopanga kufanya ziara anapaswa kujipanga kwa sababu lina kata 21 ambazo zipo mbali na makao makuu ya halmashauri.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo, Filimon Magesa alipokuwa akiongea na waandishi wa habari mjini Namtumbo alisema Wilaya ya Namtumbo kijiografia ni kubwa, lakini kwa sasa maombi ya wananchi ya kutaka kuligawa yanapaswa kufuata taratibu kupitia vikao halali vya baraza la madiwani na baadaye yanapaswa yapelekwe kwenye Kamati ya Ushauti ya Mkoa (RCC) na baadaye yatafikishwa kwenye mamlaka husika ikiridhia jimbo hilo litagawanywa.

Halmashauri ya Namtumbo ina jimbo moja la uchaguzi tofauti na maeneo mengine ya utawala wa serikali za mitaa ambayo huwa na majimbo zaidi ya moja.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Selemani Jafo (kushoto), akipata maelezo ya uzalishaji wa viuadudu wanaoangamiza viluilui wa mbu kutoka kwa Kaimu Meneja Uzalishaji wa kiwanda cha Shirika la Maendeleo ya Taifa (NDC), Kibaha mkoani Pwani jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Jafo akemea viongozi miungu watu

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Selemani Jafo, amekemea viongozi miungu watu kwenye wizara hiyo na kutaka wanaoshaurika na wenye kusikiliza mawazo ya wengine.

Aliyasema hayo jana wakati wa kikao kazi baina yake na wakuu wa taasisi zilizo chini ya wizara hiyo na wenyeviti wa bodi hizo katika ofisi za Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (TANTRADE) jijini Dar es Salaam.

Alisema baadhi ya viongozi wamejigeuza kuwa miungu watu kwenye baadhi ya ofisi na wanachotaka ndicho kinachofanyika hata kama hakina manufaa yoyote kwa wizara.

Aidha, alisema anataka kuona viongozi wanashirikisha wenzao katika kufanya maamuzi ya masuala mbalimbali na kuachana na udikteta wa kufanya kila jambo kwa wanavyoona wao.

"Kuna watu wakipata nafasi basi wanajiona wao ndiyo kila kitu hawataki kusikiliza wenzao wanasema nini, huyo unayemdharau kesho unaweza kukuta ndiye bosi wako kwa hiyo ukiwa kiongozi sikiliza na wenzako wanasema nini," alisema.

Kwa mujibu wa Jafo, hata baadhi ya taasisi zilizo chini ya wizara hiyo zimekuwa na uhusiano mbaya na wizara hali ambayo alisema inachangia kudhoofisha maendeleo yaliyopangwa na kwa wakati.

Aidha, Jafo aliwataka viongozi wa taasisi za wizara hiyo kufanyia kazi hoja zilizotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ili kutorudia makosa yaliyofanyika kwenye kaguzi zinazokuja.

Alisema hoja nyingi za CAG zinahusisha matumizi ya fedha na wakuu wa taasisi wanatakiwa kusimamia vyema ili kupata hati safi wakati wa ukaguzi.

"Sitapenda kuona hati chafu kwenye kaguzi zinazokuja nawaomba wenyeviti wa bodi mkasimamie kwa umakini sana na Katibu Mkuu naomba unipe hoja zilizotolewa kwenye kila taasisi ili wizara iangalie tumekosea wapi turekebishe," alisema.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Exaud Kigahe alisema, sekta ya viwanda ni kiungo muhimu katika ukuaji wa uchumi wa nchi hivyo ni muhimu kuendelea kuiwekea mazingira mazuri.

Alisema kuna umuhimu wa kuweka mipango thabiti kuhakikisha mazao yanayozalishwa nchini yanaongezewa thamani kabla ya kuuzwa ili kulinda viwanda vya ndani na ajira za Watanzania.

Waziri Kigahe alimpongeza Waziri Jafo kwa namna alivyoanza kazi kwa kasi ndani ya wizara hiyo na kumhakikishia kuwa watumishi wameahidi kumpa ushirikiano.

"Waziri tunajua unakwenda kwa kasi kubwa sana ndani ya muda mfupi tu tumeona kasi yako na sisi tunakuahidi tutajitahidi kwenda na kasi yako kuhakikisha sekta ya viwanda inakua na kusaidia kwenye ukuaji wa uchumi," alisema Kigahe.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Milioni 10 watibiwa na madaktari kutoka China

**Na Frank Monyo**

WATU milioni 10 wamenufaika na huduma za matibabu zinazotolewa na timu ya madaktari kutoka China katika kipindi cha miaka 60 iliyopita.

Kiongozi wa timu ya madaktari 27 wa China, Dk. Zhang Jungiao, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akielezea mafanikio yaliyopatikana tangu kundi la kwanza la madaktari hao kuwasili nchini kwa mara ya kwanza mwaka 1964.

Alisema timu hiyo ina madaktari bingwa wa upasuaji wa moyo, matibabu ya wagonjwa mahututi, dawa ya usingizi, watoto, mifupa na upasuaji wa neva.

Dk. Jungiao alisema mafanikio hayo yamekuja ikiwa ni maadhimisho ya miaka 60 ya ushirikiano wa China na Tanzania katika sekta ya afya.

Alisema katika ushirikiano huo timu ya madaktari hao ilitoa uzoefu wao pamoja na kutoa mafunzo kwa madaktari wa Tanzania jinsi ya kutumia vifaa vipya vya kisasa kutoa huduma bora za afya.

"Tulifanya jitihada za makusudi ili kuziba pengo hilo kwa kubadilishana ujuzi kwa madaktari na wauguzi wa ndani (Tanzania), ili kuokoa maisha ya Watanzania kwa kuhakikisha utoaji wa huduma za afya za hali ya juu na za kiwango zinatolewa," alifafanua.

Daktari Bingwa wa upasuaji wa moyo, Liu Yimin, kutoka katika timu hiyo alitoa wito kwa Watanzania kufanya uchunguzi wa mara kwa mara wa afya zao, ili kugundua ugonjwa kwa wakati na kupata matibabu mapema ili kuepukana na vifo.

Alisema katika kambi za matibabu zilizofanywa na timu hiyo wamebaini kuwa wagonjwa wengi waliowapatia matibabu, wamechelewa kuchukua hatua ya kufanya uchunguzi wa magonjwa ambapo wengi wao walikuwa katika hatari ya kupoteza maisha.

"Magonjwa madogo madogo yamekuwa tatizo kubwa, na pia watu wengi wana magonjwa ya kuzaliwa au urithi ambayo yanahitaji kuonana na daktari mara moja," alisema.

Dk. Yimin pia aliwataka Watanzania kuwa na utamaduni wa kula mlo kamili na kubadili mtindo wa maisha ili kuzuia ongezeko la watu wanaoripotiwa kuugua magonjwa yasiyoambukiza (NCD).

"NCDs zinaongezeka nchini Tanzania. Kwa hivyo, ni lazima tuepuke maisha yasiyofaa kama watu binafsi au familia ili kujiepusha na magonjwa," alisema.

Akitoa uzoefu wa China, ugonjwa wa moyo na mishipa uwapata zaidi watu wenye umri wa miaka 70 hadi 80 wakati Tanzania ugonjwa huo unawapata sana vijana wenye umri wa miaka 25 hadi 35.

Hata hivyo, Dk. Yimin aliipongeza Serikali ya China na Tanzania kwa mpango wa kuanzisha taasisi ya magonjwa ya moyo nchini na kuongeza kuwa imekuwa kituo kikubwa na cha juu zaidi cha uchunguzi na matibabu ya magonjwa ya moyo Tanzania na hata Afrika Mashariki.



Baadhi ya mabaki ya vibanda zaidi ya 100 vya wafanyabiashara wa soko kuu la Wilaya ya Masasi, mkoani Mtwara, baada ya kuteketea kwa moto na kuunguza bidhaa zote usiku wa kuamkia jana. **PICHA: HAMISI NASRI**

# Serikali yaanza uchunguzi moto ulioteketeza soko kuu

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

SOKO Kuu la Wilaya ya Masasi, mkoani Mtwara, maarufu Soko la Mkuti, lililoko Kata ya Mkuti, limeteketea kwa moto na kuteketeza vibanda zaidi ya 100 vya wafanyabiashara.

Moto huo uliibuka saa nne usiku wa kuamkia jana. Chanzo chake hakijajulikana.

Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Kanali Patrick Sawala alifika sokoni huko jana na kujionea hali halisi, akiwapa pole wafanyabiashara hao na kuahidi serikali itatoa majibu ya chanzo cha moto huo.

Kanali Sawala alisema serikali inawapa pole wafanyabiashara hao wa Wilaya ya Masasi kwa kupoteza mali zao, akiwaomba kuwa wavumilivu katika kipindi hiki kigumu wakati serikali ikiunda kamati maalum ya kuchunguza chanzo cha moto huo.

"Sisi serikali tunatoa pole sana kwenu kwa hasara hii mliopata na tupo pamoja na ninyi, tunachoomba muwe pamoja na tushirikiane katika kuchunguza hili," alisema Kanali Sawala.

Mwenyekiti wa soko hilo, Abdallah Mtandama alisema vipanda zaidi ya 100 vya wafanyabiashara vimeteketea kwa moto na sehemu kubwa ya biashara za wafanyabiashara zimeteketea kabisa kwa moto.

Alisema kuwa viongozi wa soko walipata taarifa usiku kuwa soko linaungua na hata walipofika walikuta tayari moto ni mkubwa na bidhaa zinaungua moto.

Musa Rashid, mfanyabiashara wa vyakula na samaki katika soko hilo, alisema bidhaa zake zote zimeteketea kwa moto.

Aliomba serikali kufuatilia kwa undani chanzo cha moto huo katika soko hilo kwa kuwa hii ni mara ya pili kunakuwa na tukio la aina hiyo, likitanguliwa na la mwaka 2016.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Mtwara, Oisa Singili alisema wametimiza wajibu wao na kwamba walifanikiwa kuuzima moto huo.

Alisema hakuna kifo wala majeruhi kutokana na moto huo, lakini mali za wafanyabiashara ziliteketea kabisa kwa moto. Alitoa pole kwa kundi hilo kutokana na tukio hilo.

Mbunge wa Masasi Mjini, Geofrey Mwambe pia aliwapa pole wafanyabiashara hao na kuahidi kuwa nao bega kwa bega kuhakikisha wanarejea kwenye shughuli zao.

# Matumizi gesi kukabili nishati chafu

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya PanAfrican Energy Tanzania (PAET), imetoa mitungi ya gesi ya kupikia pamoja na vichwa vyake itakayogawanywa kwa wananchi walio hatarini kwa kutumia nishati chafu.

Mpango huo ni sehemu ya mkakati wa taifa kujenga matumizi ya mifumo safi, salama na bora ya kupikia iliyoanzishwa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya kupunguza matumizi ya nishati chafu.

Mchango huo utagawanywa katika mikoa ya Mara, mitungi 200 na 100 kwa mikoa ya Dar es Salaam, Arusha na Dodoma na kila mkoa kupata 100.

"Ikiwa na historia ya miaka 20 ya shughuli za gesi katika kisiwa cha Songo Songo, PAET imedhamiria kutoa nishati salama, safi, inayotegemewa kwa matumizi ya kuzalisha umeme, matumizi ya viwandani, usafiri na masoko mengine," alisema.

Alisema kampuni hiyo imejikita kuhakikisha athari zitokanazo na shughuli zake kwa mazingira ni madogo iwezekanavyo na kuwa na nafasi muhimu katika mkakati wa Tanzania kuwa na uchumi msafi zaidi.

Mitungi hiyo ilikabidhiwa rasmi kwa Mbunge Janeth Masaburi mbele ya Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Hamisi Hamza Chillo, aliyemwakilisha Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Doto Biteko.

Akizungumza katika hafla hiyo, Waziri huyo alisema: "Tunamshukuru mheshimiwa Rais Samia kwa kazi kubwa anayofanya kuhakikisha tunatumia nishati safi, pia amekuwa kinara barani Afrika kwa kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia kumtua mama kuni kichwani," alisema.

Aidha, Masaburi alieleza furaha yake kwa mchango huo akisema: "Kipekee nipende kumshukuru mheshimiwa Rais kwa mpango huu wa nishati safi ya kupikia ili watu waondokane na vifo vitokanavyo na nishati chafu."

Kaulimbiu ya mpango huo ni "Masizi Tupa Kule" Rais alikuja na mpango huu ili kumtua mama kuni kwa matumizi ya nishati mbadala ya kupikia.

"Na mimi nimeamua kumsaidia kwa kutoa hamasa kwa jamii hususani kwa kinamama waweze kutumia nishati safi waachane na matumizi ya kuni na mkaa," alisema.

"Nipende kutoa shukrani zangu za dhati kwa wafadhili wetu wakiwamo mfadhili mkuu STAMICO na PanAfrican Energy Tanzania wameweza kutushika mkono kuhakikisha tunafanikisha suala letu."

Alisema pia kwa kuendana na mpango wa kitaifa wa nishati safi ya kupikia ulioanzishwa na Rais Samia, PAET inaona mchango huu kuwa kielelezo cha dhamira yake kuboresha maisha ya Watanzania kwa kuchangia nishati safi ya kupikia, PAET inasaidia matokeo chanya ya afya na mazingira katika jamii.

Zaidi ya kuchangia kampeni ya taifa ya nishati safi ya kupikia, PAET imekuwa ikiwekeza kwa miaka kadhaa katika miradi tofauti kisiwa cha Songo Songo na wilayani Kilwa.

Miradi hii ikiwa ni pamoja na uwekezaji mkubwa kwenye sekta za elimu na afya inaendana na dhamira ya PAET kuboresha hali za jamii zinazoizunguka.

Meneja wa Uwajibikaji kwa Jamii wa PAET, Andrew Kashangaki, alisema: "Tuna furaha kubwa kuchangia mkakati huu wa kitaifa wa nishati safi ya kupikia na kuchangia kuboresha hali za jamii za Kitanzania. Tunaichukua kuwa wajibu wetu kusaidia mipango ya serikali na Wizara ya Nishati katika jambo hili."



# Watakiwa kupinga ukatili wanawake, watoto

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

SHEIKH Shafi Nina wa Taasisi ya Koja Shia Ithna Asheri Jamaat (KSIJ) ya Tanga amewataka waumini wa dhehebu hilo kujitokeza kupinga ukatili dhidi ya wanawake na watoto ili kutokemeza vitendo hivyo kukithiri nchini.

Amesema waumini wa dini hiyo hawawezi kujitenga na vita dhidi ya mapenzi ya jinsia moja kwa kuwa hawakubaliani nayo.

Alikuwa akizungumza juzi katika Jiji la Tanga wakati wa maadhimisho ya kumbukizi ya siku ambayo Mtume, Hussein ibn Ally, aliuawa kikatili katika mji wa Karbala nchini Iraq.

Mtume huyo, aliuawa wakati akitetea haki za binadamu, ndio maana Koja Shia Ithna Asheri Jamaat, hutumia siku hiyo kulaani ukatili wa kijinsia katika Mkoa wa Tanga.

"Kuhusu haya mambo ya ushoga, hiki kipindi tunachoishi sasa, ndiyo hasa cha kuitumia dini zaidi kupambana na jambo hili. Kwa kuwa hakuna suluhisho isipokuwa ni dini.

"Na dini zote za mbinguni zinapambana na jambo hili, na hata tukiishi katika jamii zetu za Kiafrika, hali hii ni ngumu sana. Dini zote ziamke kupambana, ndiyo tuweze kuokoka kwa sababu tukiziangalia jamii zetu zinapotea."

Mwenyekiti KSIJ-Tanga, Samir Bandal, akitoa nasaha zake katika maadhimisho hayo, alisema tukio la kuuwawa Mtume Hussein, limewafundisha mambo ambayo yapo kwenye maisha ya kila siku ya binadamu, na kwamba Uislamu ni amani na sio vita.

"Hii siku ya Ashuraa, inatukumbusha kulinda Uislamu, kuishi kwa uhuru na amani lakini pia Imamu Hussein alikwenda Kalbara siyo kwa nia ya vita bali alifuata amani," alisema Bandal.

**Amesema waumini wa dini hiyo hawawezi kujitenga na vita dhidi ya mapenzi ya jinsia moja kwa kuwa hawakubaliani nayo.**

# H'shauri zatumia mamilioni mafuta ya wenye ulemavu wa ngozi nchini

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SERIKALI imetoa ripoti maalum ikionesha halmashauri 184 nchini zilitenga Shilingi milioni 96 kwa mwaka jana kununua mafuta ya kujikinga na mionzi ya jua kwa jamii ya watu wenye ulemavu wa ngozi (albino).

Ripoti hiyo iliyotolewa juzi na Mkurugenzi wa Huduma za Jamii, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), anayeshughulikia Makundi Maalum, Amina Mfaki, inaonesha fedha hizo zilitokana na mapato ya ndani ya kila halmashauri nchini.

Akizungumza katika Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, Mfaki, alisema walionufaika na mpango huo ni albino 2,960.

Alisema kundi la watu hao, lina changamoto za ngozi na kuisukuma serikali kuwatambua na kuwakinga na athari za mionzi kwa kutumia mafuta hayo.

"Niombe kila mahali unapomuona mtu mwenye ualbino, jaribu kuona je, anatumia losheni (mafuta) ya kujikinga na mionzi ya jua? na kama hana uelewa huo, jitahidi kumuelimisha na umuelekeze kituo cha huduma za afya ili aweze kupata losheni," alisema na kusisitiza kuwa:

"Asipopata hiyo losheni akapigwa na jua, akaathirika, matokeo yake ni mabaya kwa kuwa atauguа kwa muda mrefu saratani ambayo husababisha kifo."

Mfaki aliendelea kusema kuwa kila mwenye ulemavu na changamoto zake, serikali ni lazima izitambue na kuona namna ya kusaidia kukabiliana nazo.

Kuhusu utambuzi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, inaeleza: "Kwa utekelezaji ambalo ni jukumu kubwa la TAMISEMI, inaporatibu na kusimamia utekelezaji kwa mwaka 2022/23/24, watu wenye ulemavu waliotambuliwa ni 154,844.

"Kati yao wanawake ni 76,178 na wanaume 78,666, ambao walitambuliwa na kufanyiwa tathimini. Lakini, kupewa huduma za mahitaji mbalimbali, vikiwamo vifaa saidizi vilivyotolewa kwa watu wenye ulemavu."

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, serikali iligawa miwani kwa watu wenye uoni hafifu na miavuli kwa kundi la wenye ualibino 1,100 kwa mwaka 2023/24 hadi kufikia Februari mwaka huu.

Katika ripoti hiyo, wenye ulemavu waliogawiwa fimbo nyeupe walikuwa 700, kofia 8,456 zikitolewa na vifaa saidizi kwa walemavu wa viungo waliopewa baiskeli za miguu mitatu 2,931.

Serikali kwa kutumia sheria za watu wenye ulemavu, imeelekeza kuundwa kamati zao ngazi ya mikoa.

Kamati hizo zina wajumbe mchanganyiko wa watu wenye ulemavu na wasio na ulemavu.



Kaimu Katibu wa kikundi cha madereva wa mabasi Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Mohamed Phonza (kushoto), akitoa maelekezo ya utaratibu wa ufanyaji kazi kwa madereva katika stendi kuu ya mabasi wilayani humo jana asubuhi, ambapo kwa sasa wameboresha kikundi hicho kwa kuwa na sare na vitambulisho. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mabadiliko tabianchi 'pasua kichwa'

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAWAKILISHI wa mashirika na taasisi kutoka mataifa barani Afrika wanajadili njia bora za kuhifadhi baioanuai kwa kutumia utamaduni wa asili katika jamii ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

Akifungua mkutano wao wa siku tatu unaofanyika katika Kituo cha Maendeleo na Ushirikiano wa Kimataifa (MS TCDC) jana jijini hapa, Mwenyekiti wa Bodi ya Envirocare, Dk. Monica Kagya, alisema mradi huo unatekelezwa na Mtandao wa Afrika wa Kuhifadhi Bayoanuai (ABN) kwa kipindi cha miaka 11 katika nchi 11 za Afrika ikiwamo Tanzania.

Dk. Kagya, alisema lengo la kufanyika kwa mkutano huo ni kubadilishana uzoefu katika utekelezaji wa mradi huo muhimu ukihusisha jamii katika uhifadhi wa baioanuai kupitia mila na desturi za jamii.

"Tumeona jamii wana njia za asili za kuhifadhi baioanuai, hivyo tunataka watumie njia hizo ili zisiweze kupotea na baioanuai hizo tunazozungumzia ni upande wa vyakula, wanyama, mimea na mazingira," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Kagya, mradi huo unashirikisha vijana na wanawake kwa kuwa ni makundi muhimu ambayo yataweza kuendeleza teknolojia hiyo ya asili na kunusuru isipotee.

"Teknolojia za asili ni nzuri tunapaswa kuzilinda ndio sababu mradi huu unajaribu kuangalia ni njia gani zilizo bora tuweze kuziandika, kuzihifadhi na kuzisambaza kwa jamii zote Ulimwenguni ili zitumike na kuchangia uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi," alisema na kuongeza:

"Jamii imepokea suala hili vizuri kwa kuwa ndio waathirika wa kwanza baioanuai ikipotea," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya ABN, Dk. Sulemana Abudulai kutoka nchini Ghana, alisema kwa kipindi cha miaka 20, mradi huo umetekelezwa katika nchi mbalimbali za Afrika.

Dk. Abudulai, alisema kwa kipindi hicho, wamefanya kazi na wananchi katika jamii kwa kuangalia njia bora za kuhifadhi baioanuai kwa lengo la kuhifadhi mazingira.





# Maofisa ardhi matatani kwa rushwa

**Na Vitus Audax,**
MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda, amemwagiza Kamanda wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani hapa kuwakamata maofisa wawili wa Idara ya Ardhi wa Manispaa ya Ilemela kwa tuhuma za kuomba rushwa.

Mtanda alitoa agizo hilo juzi katika Mtaa wa Igoma wakati wa mkutano wa kusikiliza na kutatua kero za wananchi baada ya kuibuka madai ya maofisa hao kuomba rushwa wanapotoa huduma za upimaji viwanja kwa wananchi.

Mwananchi, Matiko Migire, akiwasilisha kero yake katika mkutano huo alidai kuwa maofisa hao walimwomba rushwa ya Shilingi milioni 2.43 kwa ajili ya kumpimia viwanja namba 311, 312 na 313 Block 'A' Pasiansi.

Magire alitoa madai hayo huku akiwa na viambatanisho vya ushahidi wa mawasiliano yake na maofisa hao kwa njia ya mtandao wa WhatsApp kuthibitisha kuombwa kulipa fedha kwa namba ya malipo ya serikali ya 'contral number' na kingine mkononi kinyume cha sheria.

**Akijibu madai hayo, Mtanda alisema kitendo hicho si cha kiungwana na kinawanyima haki wananchi, wakati TAKUKURU wanachunguza, idara ya ardhi ilipewa siku saba kukamilisha upimaji viwanja hivyo.**

Matiko aliendelea kudai kuwa mwaka 2019, halmashauri hiyo iliomba hati za viwanja hivyo na kuzifuta, kisha kuahidi kufanya upimaji mwingine na wamiliki wake, Joseph Mashiku, Hezeline Chawachi na Desderius Ntobi kuwapa namba ya kulipia gharama ya Shilingi 500,000.

Alidai idara hiyo haijawahi kutekeleza ahadi ya kwenye viwanja hivyo na badala yake wamekuwa wakimtafuta kwa simu mmoja wa maofisa hao na kumtaka atume kiasi hicho cha Sh.milioni 2.43 ikiwa fedha halali anayotakiwa kulipia ni Shilingi 500,000 tu.

Akijibu madai hayo, Mtanda alisema kitendo hicho si cha kiungwana na kinawanyima haki wananchi, wakati TAKUKURU wanachunguza, idara ya ardhi ilipewa siku saba kukamilisha upimaji viwanja hivyo.

Akizungumzia kero ya maji kwa baadhi ya mitaa ya Nyamagana, Mtanda alisema kupitia mkopo wa Sh. bilioni 400 kutoka Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD), Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) itasambaza huduma hiyo umbali wa zaidi ya kilomita 700 kutoka chanzo cha Butimba hadi kwenye maeneo hayo.



Mwinjilisti Ezekiel Odero (kulia) wa Kanisa la Newlife Prayer Center kutoka Mombasa nchini Kenya, akiuombea Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza jana, baada ya kuukagua ikiwa ni maandalizi ya mkutano wa injili unaotarajia kufanyika Julai 24 hadi 28, mwaka huu. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# Mwinjilisti awaasa Watanzania kudumisha amani

**Na Neema Emmanuel,**
MWANZA

MWINJILISTI wa Kanisa la Newlife Prayer Center and Church kutoka Mombasa nchini Kenya, Ezekiel Oderoamewataka Watanzania wasikubali kuvurugwa na uchaguzi ili kulinda na kudumisha amani na umoja nchini.

Odero alitoa wito huo juzi jijini hapa, wakati wa ukaguzi wa uwanja wa CCM Kirumba ikiwa ni maandalizi ya mkutano wa injili unaotarajia kufanyika kuanzia Julai 24 hadi 28 mwaka huu.

Alisema amani, upendo na umoja nchini vinatakiwa kulindwa kwa sababu havinunuliwi huku akitoa mfano wa baadhi ya mataifa duniani kupoteza amani kufuatia vurugu za uchaguzi.

Akizungumzia kuhusu utalii, Odera, alisema unategemea hali ya usalama wa nchi iliyopo, hivyo zikiwepo vurugu za aina yoyote, idadi ya watalii wanaotembelea vivutio, inapungua kwa kuhofia kupoteza maisha.

Akizungumzia kuhusu mkutano huo wa injili, alisema maelfu ya watu wanatarajiwa kuwasilia mkoani hapa, wengine kutoka nchi za nje.

Mwinjilisti huyo, alisema ameubariki uwanja huo na yeyote atakayekanyaga ardhi yake, Mungu amtendee jambo ambalo litabaki kuwa kumbukumbu.

Alitoa hamasa kwa wagonjwa na watumishi wa Mungu wanaotarajia kupata uponyaji wasiache kutumia dawa na kudai kuwa Yesu anapoponya wala hakukataa watu kupata tiba hospitalini.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda, alisema Rais Samia Suluhu Hassan na viongozi wengine wanaamini katika sala na msaada wa Mungu.

**Alisema kwa Jiji la Mwanza unatarajia kuboresha baadhi ya masoko ya chakula likiwemo la Buhongwa ambalo litajengwa upya na kupangiliwa kukabiliana na hali ya uchafu.**

Mtanda, alisema anajivunia uwepo wa kiongozi huyo wa kiroho, ujio wake unafungua fursa katika mkoa huo na kuwahakikishia usalama na utulivu katika kipindi chote cha mkutano huo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Wilbrod Mutafungwa, alisema jeshi hilo linatambua ukubwa wa tukio hilo, na kuwahakikishia kuwa mkoa upo salama na kuahidi kuendelea kuimarisha ulinzi.

# Serikali 'yamkalia kooni' mkandarasi Bandari ya Bukoba

**Na Restuta Damian,** KAGERA

SERIKALI imemtaka mkandarasi kukamilisha kwa wakati maboresho na ujenzi wa miundombinu katika Bandari ya Bukoba mkoani hapa ili kurahisisha usafirishaji wa mizigo ya wafanyabiashara ndani na nje ya nchi.

Kauli hiyo imetolewa juzi na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Balozi Dk. John Simbachawene, baada ya kamati ya kitaifa ya uwekezaji na biashara kukagua ujenzi huo katika bandari hiyo iliyopo katika Ziwa Victoria.

Balozi Simbachawene, alisema licha ya tatizo la kuwapo kwa miamba na kina cha maji kwenye eneo hilo ni vema kuchukua hatua kukamilisha kazi hiyo kwa wakati kulingana na mkataba baina yake na serikali.

Mkandarasi wa Mamlaka ya Bandari Bukoba, Mhandisi Mnanka Maginga, alisema shughuli zinazofanywa ni ujenzi wa kizuizi cha upepo ili meli zinazoingia ziweze kufika haraka.

Maginga alitaja shughuli nyingine kuwa ni kuongeza eneo la maegesho, ujenzi maegesho ya magari kuanzia 60 hadi 80, ukarabati wa maghala na kuongeza mifumo ya umeme.

Hata hivyo, alisema kuna vikwazo vilivyochelewesha kukamilika kwa ukarabati huo, hivyo kulazimika kuongeza miezi miwili na kukamilisha ndani ya miezi 20 badala ya 18.

"Moja ya vikwazo hivyo ni pamoja na kuongezeka kwa kina cha maji, kupatikana kwa mwamba eneo ambalo linajengwa gati la meli na kufanya kuchukua hatua za kutafuta makandarasi wa Kichina kusaidia katika maeneo hayo," alisema.

Meneja wa Bandari hiyo, Ramadhan Msuya, alisema ujenzi wa mradi huo ambao umefikia asilimia 63 za utekelezaji, unatarajiwa kukamilika Septemba mwaka huu.

Kwa mujibu wa Msuya, ujenzi wa mradi huo ambao bado unaendelea kwa upande wa miundombinu, hadi sasa umegharimu Shilingi bilioni 20.

**Mkandarasi wa Mamlaka ya Bandari Bukoba, Mhandisi Mnanka Maginga, alisema shughuli zinazofanywa ni ujenzi wa kizuizi cha upepo ili meli zinazoingia ziweze kufika haraka.**

ama
ALHAMISI JULAI 18, 2024
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 13

**DK. CHIBWE NA TIMU YAKE...**
**Kambi Fistula yaanika magumu ya wagonjwa, ikiwaachia neema maisha mapya kinamama 24**



**AKIDAI DANADANA YA MWAJIRI...**
**Mwalimu aliyeibukia Kambi ya Makonda, asimulia shida akili 'imesomba' ajira yake**

Ukurasa 12

## WIKI YA SAMIA NYANDA ZA JUU...

# Ashuhudia 'live' ndoto tiba hospitali ya wana- Katavi aliyoanza kwa 'kuokoteza'

•Nkasi azindua, akipata makubwa ya matabibu

**Na Mwandishi Wetu**

HOSPITALI ya Rufani Mkoa Katavi ni mradi mpya na mkubwa. Dhana ya utekelezaji wake ilianza mwaka 2019 na hadi kufika 2021, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akitunukiwa urais kutoka Makamu Rais; hatua ya ujenzi ilikuwa asilimia 43, kwa mujibu wa ripoti zilizoko.

Mnamo Aprili mwaka huu akiwa ziarani mkoani Rukwa, Katibu Uenezi na Itikadi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Amos Makalla, akatamka Rais Dk. Samia alikuwa katika hatua nzuri kukamilisha ahadi alizopokea kutoka kwa mtangulizi, Hayati Dk. John Magufuli. Itakumbukwa, wakati anaingia madarakani, Rais Dk. Samia, akaahidi kusimamia na kuendeleza miradi yote kitaifa aliyoacha mtangulizi, Dk. Magufuli.

Leo hii ni miaka mitatu na robo ya Rais Dk. Samia, sasa anahitimisha ahadi na matamshi yake, mojawapo ni mapinduizi makubwa kuhuisha uwapo wa Hospitali ya Rufani Mkoa Katavi,

Ilikuwa wikiendi iliyopita ziarani mjini Mpanda, akamwaga sifa kwa alichokiona katika hospitali hiyo, hata kuwapa sifa ni wa kuigwa na hospitali zingine nchini

"Nimesimama kuelezea furaha yangu, nimefika kukagua hospitali na kuona inavyoendelea," anasema Rais Dk. Samia, akisifu kwa nafasi ya upekee usafi wake, anampongezaa Mganga Mfawidhi wa Hospitali, Dk. Serafin Patrice na menejimenti yote...



Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Katavi. **PICHA: MTANDAO.**

"Hospitali hii imenipa faraja. Wakati naongozwa kuangalia madaktari wote niliofuatana nao ni vijana ambao wangependa kuhudumu kwenye miji mkubwa kama Dar es Salaam, Arusha au Mwanza.

"Lakini, vijana wazalendo wamekubali kukaa Katavi na kuhudumia wananchi, hongereni sana," anapongeza Rais Dk. Samia.

Kuhusu fedha ujenzi awamu ya pili ya mradi, Rais Dk. Samia anasema zimeshafika na kutaendelea kujengwa majengo zaidi, kuhakikisha wananchi wa Katavi na mikoa jirani wananufaika na uwekezaji mkubwa wa kiserikali.

Rais Dk. Samia akawaahidi kwamba, Serikali ya Awamu ya Sita itaendelea kuzisogeza huduma za afya karibu na wananchi na utoaji wa huduma bora, kwani ndio lengo lake kuhakikisha matibabu yanapatikana ngazi ya msingi, mpaka taifa.

Kwa mujibu Sera ya Afya ya Msingi (MMAM), kila kata kitongoji kinakuwa na zahanati na kituo cha afya kwa kila kata, huku wilaya inaakuwa na hospitali yake, mkoa unabaki kuwa na hospitali ya rufani.

Pia, juu kuna ngazi Hospitali ya Rufani Kanda, kama ilivyo Mbeya na Hospitali ya Taifa Muhimbili, Jakaya Kikwete na MOI za Dar es Salaam, pia Benjamin Mkapa ya Dodoma.

**MKOANI RUKWA**

Mnamo Julai 15, Rais Dk. Samia baada ya kutoka mkoani Katavi, akaingia Rukwa alikokamilisha ziara hado jana. Aliianza na kuzindua Hospitali ya Wilaya ya Nkasi, Rukwa yenye majengo na miundombinu ya kisasa, huko Namanyere.

Ni mradi wa majengo shilingi bilioni tano, sasa ikitoa huduma bora zaidi kwa wananchi wake wilayani, hapo nako akawataka wahudumu wa afya kuendeleza moyo na tija katika kuwahudumia wagonjwa ya bila kinyongo.

Hapo akatoa mfano wa mkasa, mtoto aliyezama kwenye maji na kupatiwa matibabu ya haraka hospitalini hapo, sasa anaendelea vizuri, imewezekana kwa hospitali hiyo kuwa na vifaa vya kisasa.

**SAFARI YA MRADI**

Hadi sasa, serikali kupitia Wizara ya Afya na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Katavi, inaendeleza ujenzi wa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Katavi, kama ilivyoelekezwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa

Ilikuwa Agosti 25 hadi 27, mwaka 2021, ikaanishwa namna pande zote mbili zinavyoshiriki katika ujenzi wa hospitali hiyo, ikianishwa katika Hati ya Makubaliano (MoU) iliyotiwa saini na Katibu Mkuu Wizara ya Afya na Katibu Tawala wa Mkoa wa Katavi.

Katika Hati ya Makubaliano (MoU) iliyosainiwa jukumu kubwa la Katibu Mkuu-Afya ni kuandaa bajeti na kufuatilia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kuendeleza ujenzi pamoja na kuingia mikataba yote ya ujenzi.

Inaanishwa, Katibu Tawala Mkoa Katavi, jukumu ni kusima-

Inaendelea Uk. 12

AFYA

## AKIDAI DANADANA YA MWAJIRI...

# Mwalimu aliyeibukia kambi ya Makonda, asimulia shida akili 'imesomba' ajira yake

**Na Beatrice Shayo, aliyekuwa ARUSHA**

IKIWA sehemu ya yaliyojiri katika Kambi Tiba ya Makonda jijini Arusha, fuatilia simulizi ya aliyetibiwa, mwalimu anayesumbuliwa na shida ya maradhi akili. Endelea

"Nilitoka kazini nikajikuta siitaki hii kazi nalala nyumbani nakosa amani, naona kuna watu wananitisha, watu wa kazini kwangu wanasema vibaya napata na hofu ya kifo sikuwa najua kama nina tatizo la akili," ni maneno ya Mwalimu Ndeitoi Laizer.

Huyo amekuwa akifundisha katika Shule ya Msingi Mkapa, katika Halmashauri ya Musoma, Kata ya Bukima Kijiji cha Kastamu mkoani Mara.

Anajitambulisha kuwa mtaalamu wa masomo ya Sayansi, Hisabati na Kiingereza, anafundisha kuanzia darasa la tatu hadi la saba.

"Kutokutulia sehemu moja ninakuwa ni mtu wa kukimbia kimbia, sauti zinanitisha! Ninakuwa ni mtu mwenye hofu ya kuuawa, kila ninapokaa najiona kama sipo salama wakati mwingine nahisi watu wananisema hata nikilala usiku nahisi watu wananiongelea vibaya," anaeleza.

Mnamo Juni 30, mwaka huu, alijitokeza kwenye kambi maalum ya madaktari bingwa iliyokuwa inatoa huduma mkoani Arusha na akapatiwa matibabu.

Anasimulia namna mwaka 2018 alianza kuwa na tatizo hilo akiwa anatoka kazini, baada ya kufika nyumbani alifanya uamuzi wa kuacha kazi kutokana na vitisho alivyokuwa 'anaviona'.

Mwalimu Laizer, aliyeajiriwa katika shule hiyo Februari mwaka 2012, anasema baada ya kufika Arusha, bado wazazi wake hawakuweza kugundua tatizo lake mapema, akawa anafungwa kamba.

"Walinifunga kamba wakiwa wanadhani nimelogwa. Kuna daktari mmoja wa Hospitali Levolosi, iliyopo jijini Arusha alianza kunipatia huduma ya afya yangu na ikatengamaa," anasema.

Anasema alivyopata nafuu mwaka 2021 alirudi shuleni kwake kuendelea na kazi hakupatiwa ushirikiano, akinena akaishia kuzungushwa bila ya majibu sahihi.



Mwalimu Ndeitoi Laizer. **PICHA: BEATRICE SHAYO**

"Niliambiwa kuna barua ya kufukuzwa kazi imeandikwa, ipo kwenye faili, kwa sababu hawakuwa na taarifa zangu na hii barua haikuweza kunifikia," anasema Laizer.

Laizer anasema, mwaka jana alienda kufuatilia barua hiyo haikuwapo, akifafanua majibu halisi kuwa: "Niliambiwa kitaitwa kikao cha kunijadili taarifa zangu, zikifika makao makuu Dodoma, waniite kwao nikajieleze.

"Ndio nasubiri mpaka sasa sijapatiwa majibu na nina familia, hii changamoto imenirudia, ndio maana nikaja kuonana na wataalamu katika hii Kambi ya Makonda."

### TATIZO LAMRUDIA

"Hii hali ilinifanya nije kuonana na daktari wa kambi ya matibabu bure, baada ya mke wangu kusikia hilo tangazo akanileta Juni 29 mwaka huu, nikafanyiwa vipimo...," anaeleza.

Anasema changamoto anayopata ni kuzipata dawa alizoandikiwa, kutokana na kuwapo foleni kubwa hata inamlazimu kurudi siku inayofuata na bado hakufanikiwa kutokana na umati kuongezeka katika dirisha la dawa.

Laizer anasema, akaamua kwenda kukopa Sh. 7,000 kwa jirani yake za kuzinunua dawa hizo anazotumia sasa, akiendelea: "Hizi dawa nazitumia mpaka sasa zimenisaidia.

"Ndio maana umeona nimeweza kupangilia vizuri maelezo yangu tunavyozungumza awali hali hiyo inavyonitokea nashindwa kupangilia maelezo yangu vizuri," anasema Laizer.

### MSHAHARA KUSITISHWA

Laizer anaeleza barua ya kufukuzwa shuleni hadi sasa, hajapatiwa na mshahara ulisitishwa baada ya mwezi mmoja kuondoka kazini.

"Nakumbuka waliacha kunipa mshahara kati ya Juni au Julai mwaka 2018 baada ya mimi kuondoka ndani ya mwezi mmoja nilifutwa mshahara wangu mpaka sasa sijajua hatima yangu," anasema.

Anasema tangu mwaka jana alivyoandika maelezo, alitegemea angepatiwa taarifa ya matokeo yake, hadi sasa hakuna alichojulishwa, hata kumsababishia msongo wa mawazo.

### NAMNA UGONJWA UNAVYOANZA

Msaikolojia Tiba wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), Alex Ndagabwene, aliyempatia matibabu, akiutaja kitaalamu ugonjwa unaomsumbua mwalimu huyo.

Anasema ni kundi mojawapo katika ugonjwa wa akili, asilimia kubwa inavyojionyesha imetawaliwa na imani, ambazo sio za kweli.

Ndagabwene anafafanua, huwa anapatwa na hali ya kujiona yupo katika mateso au kujihisi kuna wanaomchunguza maisha yake.

Anaeleza ni ugonjwa unaoambatana na dalili kubwa za imani zisizo za kweli, akiamini kwa asilimia 100 ni za kweli.

"Yeye anaweza kuamini kuna watu wanamfuatilia ama wapo watu wenye lengo baya na yeye, ni imani imara isiyotikisika anayoiamini lakini jambo hilo halipo. Ni imani ya kuhisi anatendewa uovu ama yuko hatarini kuangamizwa akishaamini hilo ni ameamini," anasema.

Mtaalamu huyo, anafafanua dalili nyinginezo ni kuwa na 'maruweruwe' kuona vitu ambavyo mwingine havioni au kuona watu anaowajua, hawapo katika eneo alilopo.

Anazifafanua hisia hizo ni mtu kuona vya kutisha, mwingine hawezi kuviona, huku akisikia sauti zikimsemesha.

Kusikia sauti na hali za kutisha, ni hali anayoitaja inaweza kumsababishia kushindwa kuhudhuria matukio ya kijamii akijiona hayupo salama.

Ndagabwene anatoa mfano wa mwanafunzi, kuacha masomo ghafla akiamini kuna vitu vibaya vinaendelea dhidi yake, au anafuatiliwa na watu chuoni bila kuwa na uthibitisho sahihi.

"Anaweza kuhisi wanafunzi na walimu wapo pamoja kutaka kumfanyia kitu kibaya na kwenda kutoa taarifa hata kituo cha polisi kueleza kuna watu wanamfuatilia ila kwenye kuthibitisha kina nani hawezi kuwajua,"anasema.

Mtaalamu huyo anaeleza, mamlaka hiyo inaposhindwa kuchukua hatua kwa alichokieleza, anajenga imani nayo inashirikiana na madau tajwa, akifafanua kwa kauli:

"Kama yupo kazini ataacha na wengi wameacha shule kwa mtindo huo."

Mtaalamu huyo anasema, baadhi yao hupelekwa kutibiwa kwa mganga wa asilia au wanauombewa shida hiyo ya afya ya akili na katika uhalisia, mtu anapoacha kazi ndani ya saa 24 hadia 48 akiondoka bila ya taarifa, inaacha ujumbe umeongezeka maradufu.

### UGONGWA UNAVYOTIBIKA

Anasema ugonjwa una tiba na mgonjwa anaweza kurudi kazini kuendelea na majukumu yake, huku akitumia dawa kwa usahihi na kuhudhuria kliniki anazopangiwa.

Ngagabwene anasema kuna waliotibiwa na wanaendelea na shughuli zao, bila ya changamoto, ili mradi wanafuata maelekezo ya wataalamu.

"Matibabu yapo ya dawa ambayo yanaenda kutuliza maruweruwe ya vitu anavyoviona vya kutisha ama imani potofu iliyojengeka na kupunguza ama kuondoa sauti azisikiazo bila uwepo wa watu halisi.

"Kuna matibabu ya kisaikolojia yanayosaidia kuzitikisa zile imani

Endelea Uk. 13

## Ashuhudia 'live' ndoto tiba hospitali ya wana- Katavi aliyoanza kwa 'kuokoteza'

Inatoka Uk. 11

mia matumizi ya fedha za ujenzi kwa kuratibu na kusimamia ununuzi wa vifaa vya ujenzi, malipo ya mkandarasi na Mshauri Elekezi kupitia kamati anazoziunda, kutekelezaji mradi kila siku.

Ujenzi wa Hospitali Rufani Mkoa wa Katavi, unatekelezwa kwa awamu kama, kulingana na upatikanaji fedha.

Awamu ya Kwanza, mradi ulianza na majengo matatu; jengo kuu lenye ghorofa moja lenye Kitalu A na B la kudumia Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto; Huduma za Dharura (EMD); Wagonjwa wa Nje (OPD); Famasia; Radiolojia; Upasuaji; Uangalizi Maalumu (ICU); na jengo la Maabara.

Ujenzi wake ulianza mwezi Mei, 2018 chini ya usimamizi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Katavi na ilikuwa itekelezwe kwa wiki 48 kwa gharama ya shilingi bilioni 9.7. Ilipofika Februari 2019, mradi ulikabidhiwa kwa Wizara ya Afya ukiwa kwenye hatua ya msingi sawa na asilimia 20 ukiendelea kutekelezwa na Mkandarasi SUMA JKT kwa mfumo wa Kandarasi (Conventional Method).

Mradi huo uliendelea kutekelezwa kwa utaratibu wa kandarasi mpaka April 2021 ukiwa katika asilimia 43 ya utekelezaji ikishatumia shilingi bilioni 3.6.

Serikali iliamua kubadilisha mfumo wa utekelezaji kwenda kwenye kinachojulikana 'Force Account' ili kuharakisha utekelezaji wake.

Serikali kupitia Wizara ya Afya, ilikamilisha taratibu za ununuzi na kumpata Mhandisi Mshauri na Mshauri Elekezi - 'Crystal Consultant' na Fundi Mjenzi SUMA JKT.

Hadi sasa gharama za kukamilisha mradi zinakadiriwa kuwa shilingi bilioni 12, zikijumuisha za ufundi na kwa mshauri elekezi.

## Mwalimu aliyeibukia Kambi ya Makonda, asimulia shida akili 'imesomba' ajira yake

**Inatoka Uk. 12**

anazokuwa nazo, ama kutambua dalili zinavyoanza na kuchukua hatua mapema, bila kusahau kujifunza namna nzuri ya kutatua changamoto za kimaisha na kuepukana na vichochezi vya ugonjwa."

**SABABU ZA UGONJWA**

Ndagabwene anasema sababu za ugonjwa huo wa akili kuwa unasababishwa na vitu vitatu ambazo ni vinasaba, kisaikolojia na mazingira aliyopitia mgonjwa bila kusahau matumizi mabaya ya vilevi kama vile bangi na pombe.

Anasema, ugonjwa huo kuna wanaorithi kutoka kwenye familia na sayansi inaeleza hata mazingira magumu mtu aliyopita, yana mchango katika hali hiyo.

"Tulikuwa tunaomba uongozi wa mkoa (Mara na Arusha) kumsaidia mwalimu huyu arudi kazini kwa kufuata taratibu zinazohitajika tutashukuru kwa kuwa ugonjwa huu ulimuanzia akiwa kazini," anatamka msaikolojia.

**MKE ASIMULIA**

Mke wa mwalimu huyo, Neema Laizer, anasema anasimulia namna mume wake alivyorejea akimtamkia ameacha kazi na alivyomuuliza sababu, akamjulisha 'anahofia kifo'.

"Hakunipa taarifa kama anakuja Arusha. Nilishangaa kumuona ananiambia kaacha kazi, nikamuuliza kwanini? Akanimbia sitaki kwenda kazini, ninahofia kifo changu," anasema. Neema, anasema hawakugundua ugonjwa unaomsumbua, mpaka walipoenda hospitali na kukutana na mtaalamu aliyewapatia dawa na afya yake kurejea vizuri.

Pia anaeleza mwaka 2021, mumewe akamwambia anaenda shuleni kufuatilia kinachoendelea na hakupatiwa majibu yanayoeleweka, ikimlazimu mwaka jana kwenda kumsaidia kufuatilia kwa pamoja. Anasema, walikaa mwezi mmoja wakifuatilia wakamwambia aandike barua hakuna majibu waliyopatiwa hadi sasa na kujikuta wanaendelea kuishi katika wakati mgumu.

"Familia ina mahitaji mengi tunapata shida kupata huduma za hospitali bima tumesitishiwa kuzitumia chakula mpaka apate kibarua cha kwenda kufanya na mafundi," anasema

Neema anasema kwa sasa ana mtoto mchanga, hana biashara anayoifanya, hivyo kilio chake ni kurejea familia ipate mahitaji yake.

"Natamani angerudishwa katika nafasi yake, ili aweze kuwalea hawa watoto changamoto katika chakula mpaka 'abangaize', hii ndio inanipa shida, maana mimi sina kazi nipo nyumbani," anasema.

Aidha, anasema kwa sasa hali yake ipo vizuri angerudishwa kazini huo ugonjwa sio kwamba unamtokea kila mara, baada ya mwaka 2018 haukutokea hadi mwaka huu.

Mama huiyo anasema, kuna kipindi aliacha kutumia dawa akiwa yupo vizuri, hata akashangaa mwaka huu ugonjwa huo ukamrudia.

"Kikubwa anachokilalamikia ni kuwaza kazi yake anasema haelewi amepotezaje kazi yake hicho ndio anachokisema mara kwa mara anawasiliana na wenzake wa Musoma hawampi ushirikiano," anasema.

AFYA

DK. CHIBWE NA TIMU YAKE...

# Kambi Fistula yaanika magumu ya wagonjwa, ikiwaachia neema maisha mapya kinamama 24

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

UGONJWA wa fistula unaelezwa kuwakumba wanawake, wanaotokwa na haja ndogo na kubwa muda wote.

Hali hiyo imekuwa ikisababisha wanawake kushindwa kufanya shughuli zao mbalimbali za kiuchumi, kutokana na kukwepa aibu ya kutokwa na haja ndogo na kubwa muda wote.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Wanawake, kutoka Hospitali ya Rufani Bugando jijini Mwanza, Dk. Elieza Chibwe, akiwa katika safu ya waliopiga Kambi mkoani Shinyanga kutoa huduma ya matibabu bure ya upasuaji ugonjwa wa fistula, anautakia ni ugonjwa wa aibu na na fedheha kwa mwanamke.

Anasema tatizo la fistula ni kubwa kwa wanawake, na husabishwa na uchungu pingamizi anapokuwa mjamzito, katika uwazi unaounganisha njia ya uzazi na sehemu ya haja kubwa na ndogo, kusababisha kutokwa kinyesi na mkojo muda wote.

"Matibabu ya fistula ni upasuaji tu, na tunataka hadi kufikia 2030 tatizo la Fistula liwe limekwisha kabisa," anasema Dk. Chibwe.

**MGONJWA ANENA**

Mwanamke mmoja (jina tunalo), anaelezea namna ugonjwa huo fistula ulivyomtesa ndani ya miaka 38, akisema kwa kipindi hicho hajaweza kufanya shughuli za kumuingiza kipato, akikwepa aibu hiyo kutokwa na haja kubwa na ndogo muda wote.

Anasema ilifikia kipindi haja kubwa inaanza kutoka, hivyo akaishi kwa tabu, huku mwanamke mwingine anasema yeye alipatwa na tatizo hilo la mwaka 1995, na kwamba muda kidogo mume wake alimkimbia, kutokana na kushindwa kuvumilia tatizo lake.

"Ugonjwa huu ni mbaya sana una mdhalilisha mwanamke na ulifanya mume wangu akanikimbia na kunitekeleza, uzuri tatizo hili lilinipata katika ujauzito wangu wa pili na mtoto alifariki na sasa nina mtoto mmoja wa kwanza ambaye ndiye ananisaidia na kuniuguza," anasema.



Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Shinyanga, Dk. Luzila John akisikiliza ushuhuda wa aliyefanyiwa upasuaji. **PICHA: MARCO MADUHU.**

> **"Tunashukuru Kambi hii ya Madaktari Bingwa wa Magonjwa ya Wanawake kutoka Bugando, kwa kutupatia tiba ya matibabu bure ya upasuaji wa ugonjwa huu wa Fistula, na sasa hali yangu inaendelea vizuri," anaongeza.**

"Tunashukuru Kambi hii ya Madaktari Bingwa wa Magonjwa ya Wanawake kutoka Bugando, kwa kutupatia tiba ya matibabu bure ya upasuaji wa ugonjwa huu wa Fistula, na sasa hali yangu inaendelea vizuri," anaongeza.

Kambi hiyo ya Madaktari Bingwa Nane wa Magonjwa ya Wanawake kutoka Bugando, ilikaa kwa muda wa siku Tano mkoani Shinyanga, ikiwafanyia upasuaji wagonjwa wa fistula bure jumla wanawake 24.

Mwakilishi kutoka Shirika la Americares Dk. Jonas Kagwisage, wafadhili wa kambi hiyo, anasema kwa sasa wamefanya kambi hiyo kushirikiana na Madaktari Bingwa wa Magonjwa ya Wanawake wa Bugando.

Anasema wameifanya kwa muda wa siku Tano, wamefanikiwa kuwafanyia wa wagonjwa wa fistula wanawake 24, na kuwarejesha katika hali zao za kawaida.

Mratibu wa Afya ya Uzazi na Mtoto Mkoa wa Shinyanga Halima Hamis, anasema tatizo la fistula linakumba zaidi wanawake wanaojifungulia nyumbani bila ya msaada wa wataalamu wa Afya.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Shinyanga Dk. Luzila John, anasema hospitali hiyo haina daktari bingwa mtaalamu wa upasuaji wa ugonjwa wa fistula, na kwamba hao hutibiwa Bugando Jijini Mwanza.

Anasema, kupitia Kambi hiyo ya madaktari bingwa wa magonjwa ya wanawake kutoka Bugando, baadhi ya madaktari wao wamashajengewa uwezo na watakuwa wakitoa tiba hiyo ya fistula.

Diwani wa Mwaaza Juma Nkwabi Kata ambayo ipo Hospitali hiyo ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga, anaiomba serikali ipeleke madaktari bingwa katika hospitali hiyo, wa kutoa tiba ya fistula kwao.

AFYA

# Simulizi yenye utata mauaji kinamama Kenya, maswali ya umma yametawala, kuliko majibu

**Nairobi, Kenya**

KUKAMATWA kwa mshukiwa wa mauaji ya Kenya kumezua hisia kali kote nchini, baadhi ya watu wakihoji undani wake.

Polisi wanasema, Collins Jumaisi Khalusha (33), alikiri kuwaua wanawake 42, lakini siku ya Jumanne wakili wake akaiambia mahakama kuwa aliteswa ili kukiri mauaji.

Ni tukio la kutatanisha, baada ya ugunduzi wa mabaki ya miili tisa iliyokatwa vipande, kuwekwa kwenye mifuko, kufungwa kwa kamba na kutupwa kwenye machimbo ambayo hutumika kama jaa la taka karibu na Kituo cha Polisi mtaani Mukuru, jijini Nairobi.

Kuna malalamiko, baadhi ya watu hawaelewi vipi polisi hawakuweza kugundua kuwapo miili iliyotupwa wastani mita 100 kutoka waliko, Mtaa wa Mabanda wa Mukuru Kwa Njenga.

Kaimu Mkuu wa Polisi Douglas Kanja, Jumapili akatangaza kwamba, maofisa wa Kituo cha Polisi Kware, karibu na eneo la tukio wamehamishwa.

Mamlaka inayosimamia utendakazi wao, ilisema inafanya uchunguzi kubaini ikiwa polisi walihusika kwa namna yoyote na mauaji hayo.

Familia ya Josephine Owino, aliyetoweka inasema alimjia ndotoni' mmoja wao na kuwaelekeza kwenye jalala hilo.

Diana Keya, ndugu wa marehemu huyo, akasema kwamba familia iliwalipa vijana kupekua taka katika jalala hilo, hata kuibua mkasa wa kuwapo miili tisa iliyoharibika vibaya, ikipatikana Ijumaa wiki iliyopita. Ilikuwa imefungwa kwenye mifuko ya plastiki kwa kutumia kamba.

Taarifa za awali za polisi zilisema "kisa hicho kiligunduliwa na wakazi." Alipoulizwa baadaye Mkurugenzi ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai, Mohamed Amin akajibu "Sisi sio waotaji na hatuamini ndoto."

Polisi wanasema, miili iliyopatikana ilikuwa katika hatua tofauti za kuoza, hata ikiashiria waathiriwa walikuwa wameuawa kwa nyakati tofauti.

Pia, polisi wanasema mshukiwa anayeitwa Khalusha, amekiri kuwaua wanawake hao kwa kipindi cha miaka miwili, ushahidi ambalo sasa unatiliwa shaka.

Jambo lisilo wazi ni iwapo mabaki yalitupwa wakati huo au hivi karibuni. Hussein Khalid, Mkurugenzi Mtendaji wa shirika la Haki Afrika, analaumu maelezo ya polisi kuhusu matukio hayo yalikuwa na "maswali mengi".

Mtazamo huo wa maswali, pia unahusu polisi walivyofanikiwa kumkamata mshukiwa chini ya siku tatu, baada ya kupatikana miili hiyo, ingawa kabla hawakuwahi kutilia shaka tukio lolote lisilo la kawaida katika muda wa miaka miwili.



Eneo kulikofanyika mauaji. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Jumatatu wiki hii, polisi walisema Khalusha alikamatwa kwenye baa akitazama mechi ya fainali ya michuano ya Euro 2024.

Walionyesha kwenye vyombo vya habari baadhi ya vitu vinavyosemekana kupatikana kwa nyumba ya mshukiwa,- pia karibu na mahali aliko kulipatikana simu 10, vitambulisho na nguo za ndani za kike.

Polisi wanasema, walifuatilia aliko Khalusha baada ya kupata simu ya mmoja wa waathiriwa wake.

**WAATHIRIWA JE?**

Ni mwili mmoja tu uliotambuliwa hadi sasa, Roseline Ongogo mwenye umri wa miaka 24 na ndugu yake Emmanuel Ongogo, anayeeleza kwamba alitoweka Juni 28 mwaka huu, alipotoka nyumbani kwenda kutafuta kibarua.

Anasema familia yake ilienda chumba cha kuhifadhi maiti cha City, Nairobi ilipopata habari kuhusu miili iliyopatikana Mukuru.

Walimtambua, kwa sababu alikuwa na nguo aliyokuwa amevalia na msongo wa nywele aliyokuwa nayo wakati alipotoweka.

Polisi pia wanadai kuwa mke wa Khalusha, alikuwa mwathiriwa wake wa kwanza na wanasema kitambulisho chake kilipatikana, kuwa miongoni mwa vitu vingine vinavyodaiwa kuwa vya waathiriwa.

Familia ya Owino, inasema kuwa iliota kuhusu aliko na wakawa wanasubiri uchunguzi wa kipolisi.



Mtuhumiwa wa mauaji, akiwa chini ya ulinzi.

**MTAZAMO USALAMA**

Kupatikana miili hiyo kumeibua kumbukumbu ya mauaji ya kinyama ya mwezi Januari mwaka huu, ya msichana Rita Waeni aliyekuwa na umri wa miaka 20.

Mwili wake uliokuwa umekatwa vipande ulipatikana katika nyumba ya kupanga kwa makazi ya muda mfupi jijini Nairobi. Kesi hiyo bado haijatatuliwa.

Kifo hicho kilisababisha maandamano nchini kote kupinga kuongezeka kwa visa vya mauaji ya wanawake na unyanyasaji dhidi yao.

Shirika la kutetea haki za binadamu la Amnesty International, lilisema zaidi ya mikasa 500 vya mauaji ya wanawake yalirekodiwa nchini Kenya kati ya 2016 na 2023.

Ikadai miili yote iliyopatikana jalalani, saswa na mkasa wa sasa unachukua msukumo ni ya wanawake. Kuna viongozi wachache wa makundi ya wanawake wakusanyika katika chumba cha kuhifadhi maiti, waliiomba serikali kuharakisha uchunguzi na kukomesha ukatili wa aina hiyo.

Alipoulizwa polisi walikuwa wakifanya nini kushughulikia kesi za mauaji ya wanawake na unyanyasaji dhidi ya wanawake, Msemaji wake Resila Onyango, akafafanua hawezi kushughulikia suala hilo, kazi ya polisi ni "kulinda maisha na mali ya kila mtu."

• ***Kwa mujibu wa BBC.***



# Wazazi kukamatwa kukaidi kuchangia chakula shuleni

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

MKUU wa Wilaya ya Mkalama mkoani Singida, Moses Machali ameamuru wazazi wanaokataa kuchangia chakula shuleni kwa ajili watoto wao, wakamatwe na kuchukuliwa hatua kwa kukwamisha jitihada za serikali kuongeza kiwango cha ufaulu.

Machali alitoa amri hiyo juzi kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika katika Kijiji cha Mwangeza kwa ajili ya kusilikiza na kutatua kero zinazowakabili wananchi.

"Kila mzazi anapaswa kuchangia chakula shuleni watoto wasome vizuri, ambao hawatachangia wachukuliwe hatua za kinidhamu maana tunapotoa chakula tunaboresha mazingira ya wanafunzi kujifunza na hivyo kuongeza ufaulu,"alisema.

Alisema kutokana na umuhimu wa chakula shuleni, suala la kila mzazi kuchangia liwe ni la lazima kwani mkakati wa wilaya ni kuhakikisha kiwango cha ufaulu katika shule zote kinaongezeka kila mwaka.

Kwa upande mwingine, Machali amepiga marufuku mashamba ya shule kukodishwa kwa wananchi badala yake yatumike kuzalisha chakula cha wanafunzi.

"Sitaki kusikia mashamba ya shule yamekodishwa kwa watu, tumieni kulima chakula cha wanafunzi ili tuweze kupunguza hata gharama za kuchangia chakula shuleni," alisema.

Mkuu huyo wa wilaya, aliagiza kwa mara nyingine kuvunjwa mara moja kwa Kikundi cha Nkiri kwa kuanzishwa bila ya kuzingatia sheria na kuliagiza Jeshi la polisi kuwakamata watakaokiuka agizo hilo.

# Watoto 12 wapona ugonjwa selimundu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WATOTO 12 wamepona ugonjwa wa selimundu baada ya kupandikizwa uloto na kukamilisha matibabu katika Hospitali ya Kanda ya Benjamin Mkapa (BMH) ya jijini hapa.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, mmoja wa wazazi wa watoto hao, Mary Mgumia, alishukuru uongozi wa hospitali hiyo na serikali kwa matibabu hayo.

"Naishukuru serikali kugharamia matibabu ya wagonjwa wa selimundu, hii imeonyesha jinsi gani ilivyofanya uwekezaji mkubwa kwenye sekta ya afya," alisema Maria.

Alisema mwanawe huyo alikuwa anakabiliwa na maumivu ya viungo, hali ilivyozidi kuwa mbaya, alimpeleka kituo cha afya, baadaye kuhamishiwa hospitalini hapo ambako alipatiwa matibabu na kupona.

"Pale kituo cha afya tulifanya vipimo wakatuambia tuende Benjamin (Hospitali ya Benjamin Mkapa) tunaweza tukapata suluhisho," alisema Maria.

Alisema mwaka 2020, alipatiwa vipimo ambavyo vilionesha mwanawe anasumbuliwa na selimundu, akaanzishiwa dawa na kutakiwa kuhudhuria kliniki ya magonjwa ya damu.

"Daktari aliyemfanyia vipimo mwanangu aliniambia niondoe wasiwasi kwa kuwa wanatarajia kuanzisha huduma ya upandikizaji uloto ambayo inaponesha kabisa selimundu," alisema.

Hospitali hiyo juzi ilifanya upandikizaji uloto kwa mtoto Caris Anthony (8) chini ya madaktari wake bingwa.

Dk. William Lloyd wa kitengo cha upandikizaji Uloto BMH, alisema mtoto huyo atakuwa chini ya uangalizi wa kliniki ya magonjwa ya damu kwa kipindi cha mwaka mmoja.

"Ninawashukuru wazazi wake kwa kuiamini BMH kwani wangeweza kwenda nje ya nchi kupata huduma hiyo, lakini wakaja hapa," alisema Dk. Lloyd.

Aliwahimiza wazazi kuwapeleka watoto hospitalini wanapoona wana matatizo ya selimundu ili waweze kupatiwa matibabu haraka.

BMH iliyoko jijini Dodoma, inatoa tiba ya upandikizaji uloto kwa wagonjwa wa selimundu na matibabu ya magonjwa mbalimbali.



Mkuu wa Wilaya ya Mkalama, mkoani Singida, Moses Machali (kulia), akizungumza katika mkutano wa hadhara na wanakijiji wa Mwangeza juzi, wakati akisikiliza na kutatua kero zinazowakabili. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Jafo aagiza ujenzi ofisi WMA

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo, amemwagiza mkandarasi kukamilisha mradi wa ujenzi wa jengo la ofisi za makao makuu ya Wakala wa Vipimo (WMA) kulingana na mkataba ili kupunguza mzigo kulipa fedha nyingi kwenye majengo ya kukodi.

Dk. Jafo alitoa agizo hilo jana jijini hapa baada ya kukagua ujenzi wa jengo hilo.

Alisema mkandarasi huyo anapaswa kukamilisha ujenzi ndani ya muda wa mkataba ili wakala huo uondokane na gharama za kulipa fedha katika majengo ya kukodi.

"Ziara hii ni mwendelezo wa ziara zangu za kukagua taasisi zote ambazo zipo kwenye wizara hii ya Viwanda na Biashara jana (juzi) tulikuwa mkoani Pwani, leo (jana) tupo hapa Dodoma kukagua jengo la Wakala wa Vipimo," alisema.

Alisema lengo la wizara hiyo ni kuhakikisha taasisi zote zinafanya kazi zake kutoka makao ya nchi, hivyo kukamilika kwa jengo hilo kutasaidia utoaji wa huduma kwa mikoa mingine nchini.

Vilevile Jafo, aliuagiza wakala huo kuendelea kutekeleza maagizo yake aliyoyatoa hivi karibuni, ikiwemo kufanya ukaguzi wa mitaa za umeme kabla ya kufunga kwa wateja.

"Niwatake muendelee kukagua mita za umeme kabla hazijafungwa kwa wananchi ili kuwapunguzia gharama ambazo zinaweza kujitokeza kutokana na ubovu wa mita hizo,"alisema.

Mwakilishi wa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala huo, Joseph Maliti, alisema ujenzi huo ambao utagharimu kiasi cha Sh. bilioni sita hadi sasa umekamilika kwa asilimia 81.5.

"Mheshimiwa Waziri mradi huu kwa mujibu wa mkataba unapaswa kukamilika Januari 2025, tunatarajia ukamilike ndani ya muda au kabla ya hapo, "alisema Maliti.

Alisema WMA itaendelea kutekeleza maagizo yaWaziri huyo, ikiwemo ukaguzi wa mita za umeme kabla ya kufungwa kwa wateja ili kumaliza malalamiko.

Awali, Mkandarasi huyo, Mhandisi Justine Kyando kutoka Kampuni ya Mohamed Bulders, aliahidi kukamlisha ujenzi huo kwa muda uliopagwa ili wakala huo uondokane na gharama za kulipa kodi ya pango

"Kazi zilizobaki ni kumalizia kufunga umeme,mifumo ya zima moto, mifumo ya TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano) na kupaka rangi ambazo zinaweza kukamilika kabla ya mkataba kwisha,"alisema Kyando.

# 16,000 Msanga kunufaika kilimo cha umwagiliaji

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WIZARA ya Kilimo imeanza ujenzi wa bwawa katika Kata ya Msanga Halmashauri ya Wilaya ya Singida mkoani hapa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji kwa wakazi 16,000 na kujikwamua kiuchumi.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, alisema hayo juzi wakati akishuhudia hafla ya makabidhiano ya mradi huo yaliyofanyika Kijiji cha Msange kati ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Mkandarasi wa Kampuni ya Kagwa General Supplies Limited.

Dendego, alisema ujenzi wa mradi huo utakuwa ni wa sita katika miradi iliyopelekwa mkoani hapakwa gharama ya mabilioni ya fedha.

Alisema kujengwa kwa bwawa hilo kwa gharama ya zaidi ya Sh.Bilioni 17.7utakuwa mkombozi kwa wakazi haokuendesha kilimo zaidi ya mara mbili hata kipindi cha kiangazi na kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula, biashara na mbogamboga.

Dendego, alisema mradi huo utawezesha wakazi hao kulima ekari 3,500 na kwamba ili uweze kudumu kwa muda mrefu ni jukumu lao kuulinda.

Alisema serikali itahakikisha inapeleka mbegu bora za kisasa ambazo zinatakuwa zinatoa mengi zaidi na kuinua uchumi wa wakazi hao.

Mhandisi wa Umwagiliaji Mkoa wa Singida,Japheth Senyinah, alisema mradi huo pia utahusisha ujenzi wa nyumba za watumishi,miundombinu ya umwagiliaji na ununuzi wa gari kwa ajili ya wafanyakazi kusimamia mradi.

Alisema mradi huo ambao ujenzi wake unatarajia kukamilika Julai 27, mwaka 2027, utahusisha ujenzi arabara za mashambani zenye urefu wa kilomita 9.2, mfereji mkuu wa kusambaza maji mashambani wenye urefu wa mita 1,370, madaraja na mifereji midogo 6,470.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Eliya Dighah, aliishukuru serikali kwa kupeleka fedha za ujenzi wa mradi huo nakuwa mkombozi kwa wananchi kuondokana na umaskini wa kipato





# Hospitali yadaiwa kukataa kumfanyia upasuaji mtoto

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya kimeonyesha kusitikishwa na kitendo cha mtoto wa miaka miwili kukataliwa kufanyiwa upasuaji kuondoa uvimbe kwenye mkono baada ya mzazi wake kukosa fedha.

Hatua hiyo imekilazimu chama hicho kuviagiza vituo vya afya mkoani hapa kutekeleza sera ya afya kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano kutibiwa bila malipo.

Mwenyekiti wake, Patrick Mwalunenge alisema juzi kuwa baada ya kupokea taarifa ya mkazi wa Wilaya ya Kyela, Tulinagwe Mwakyelu mtoto wake kukatiliwa kupatiwa matibabu kwa kukosa fedha katika hospitali hiyo ya serikali, kiliwasilisha na wenzao wa wilayani humo na kuagiza aletwe Hospitali ya Rufani Kanda ya Mkoa wa Mbeya kwa matibabu.

Alisema taarifa hizo zilidai kuwa mtoto huyo alikuwa anakabiliwa na uvimbe kwenye mkono na kukatiliwa kufanyiwa upasuaji baada ya mzazi wake huyo kukosa Sh. 350,000 hali iliyomlazimu kurejea nyumbani bila kutibiwa.

Mwalunenge aliagiza mtoto huyo afanyiwe upasuaji na matibabu mengine katika hospitali hiyo bila malipo yoyote.

"Taarifa za ugonjwa wa mtoto huyu nilizipata kupitia kwenye mitandao ya kijamii, nikaamua kuwasiliana na viongozi wa chama wa Wilaya ya Kyela ambao wamefanya mchakato wa kumsafirisha mpaka hapa na sisi tumempokea," alisema Mwalunenge.

Alisema baada ya kufika katika ofisi ya chama hicho, alimpatia mama huyo, Sh. 400,000 kwa ajili ya kumhudumia mtoto huyo na kumtaka kumtafuta mzazi mwezie ili wasaidiane kulea watoto wao.

Tulinagwe, alisema alisema mtoto huyo alianza kuugua mwanzoni mwa mwaka jana kwa kuvimba kwenye mkono.

Alisema alianza kumtibu mtoto huyo kwa kutumia dawa za mitishamba kabla ya kwenda Hospitali ya Wilaya ya Kyela.

Alisema alipofika hospitalini hapo, walimpatia matibabu bila mafanikio, hivyo wakamwandikia kwenda hospitali kubwa zaidi kupata matibabu.

Alisema alikaa muda mrefu hospitalini hapo baada ya kupewa sharti la kutotoka mpaka atakapolipa fedha alizokuwa anadaiwa, hali iliyomlazimu kutoroka

"Huyu mtoto ni pacha, mwenzie nimemwacha nyumbani, nawalea peke yangu kwa sababu baba yao aliwakataa na akakimbia, " alisema na kuwashukuru viongozi wa CCM kwa kumsaidia kulipia gharama za matibabu.

Alisema mtoto huyo amekuwa akipata maumivu makali, kulia muda wote na kushindwa kutekeleza majukumu yake.



Kaimu Katibu Tawala Msaidizi (Utawala na Usalama wa Rasilimali Watu) Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Pwani, Peter Stephen, akizungumza na Mjumbe wa Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NACONGO), kutoka mkoa huo, Prisca Ngweshemi (kushoto), alipokwenda kujitambulisha ofisini hapo, juzi. Katikati ni Ofisa Maendeleo ya Jamii wa mkoa huo, Roseline Kimaro. **PICHA: SABATO KASIKA**

# RC apata mwarobaini wananchi, shule kugombea ardhi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani hapa imeagiza maeneo yote ya shule za msingi na sekondari yapimwe na kukatiwa hatimiliki ili kudhibiti kuvamiwa na baadhi ya wananchi kwa ujenzi wa makazi na kilimo na kusababisha migogoro.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera kwenye kikao cha wadau wa elimu.

Homera, alisema maeneo mengi ya shule mkoani hapa yamevamiwa kutokana na kutokuwa na hatimiliki.

Aliwataka wakurugenzi wa halmashauri mkoani hapa kushirikiana na wadau kupima maeneo hayo na kufuatilia taratibu za kupata hatimiliki na hilo litakuwa suluhisho la migogoro kati ya serikali na wananchi.

Homera, alisema kila mkurugenzi atatakiwa kutoa taarifa ya utekelezaji wa agizo hilo na mengine ambayo yalitolewa kwenye kikao hicho ambacho hufanyika kila mwaka.

"Maeneo mengi ya shule yamekuwa yakivamiwa kwa sababu hayajapimwa na kumilikishwa, sasa ili kudhibiti hili hakikisheni mnayapima na kuyakatia hatimiliki, tuyamiliki kisheria ili watakaovamia tuwe na pa kuwakamatia," alisema.

Baadhi ya walimu walithibitisha kuwepo kwa migogoro ya ardhi baina ya shule na wananchi na kusababishwa maeneo hayo kutopimwa wala kumilikishwa kisheria.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Anseshelo iliyopo Kata ya Iganjo Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, George Mlawa, alisema maeneo mengi hasa ya vijijini shule hazijapimwa hali hivyo kusababisha wananchi kuvamia na kufanyia shughuli zao.

Aliishukuru serikali kwa agizo hilo kuwa litasaidia kupunguza migogoro hiyo na kuzifanya shule kuendelea kuwa na maeneo makubwa kwa maendeleo na upanuzi wa miundombinu.

"Kesi za aina hii ni nyingi sana hasa maeneo ya vijijini, wavamizi huwa hawatoki mbali wanakuwa ni walewale majirani wa shule ambao wanaanza kidogokidogo kujitanua kwenye maeneo ya shule," alisema

Ofisa Elimu wa Mkoa huo, Mwalimu Kiduma Mageni, alisema ofisi yake inashirikiana na wadau kuhakikisha wanafunzi wanakuwa salama shuleni na nje ya shule.

Alisema zimeanzishwa klabu za wapinga rushwa na ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto kuhakikisha watoto wanakuwa salama wakati wote.

Alisema ofisi yake imeanzisha utaratibu wa kila shule kuwa na sanduku la maoni kwa wanafunzi kuruhusiwa kuandika madhira yanayowakuta ili yashughulikiwe.

# Mbegu za soya zafanyiwa majaribio

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole jijini hapa imeanza kufanya utafiti wa majaribio ya aina 30 ya mbegu za soya ili kupata mbegu bora na kumudu mahitaji ya soko katika nchi za Bara la Asia.

Mtafiti Mbunifu wa Mbegu TARI, Michael Kilango aliyasema hayo wakati akitoa elimu kwa wakulima ya kuongeza tija kwenye uzalishaji wa zao hlo.

Alisema waliamua kufanya utafiti huo kutokana na mahitaji ya walaji katika soko la zao hilo ambalo serikali imepata soko la uhakika nchini Chinga.

"Mbegu tunazozifanyia utafiti zinatoka katika maeneo mbalimbali nchini na katika baadhi ya mataifa ya Afrika Mashariki, kati ya mbegu hizi 30 tunatarajia tupate aina tatu ambazo tutazipeleka katika Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu (TOSCI) ili zisajiliwe," alisema Kilango.

Alisema katika msimu wa kwanza wa utafiti huo, walipata aina nne za mbegu na baada ya kukamilisha utafiti wa sasa, watafikisha mbegu saba ambazo watazisambaza kwa wakulima.

Alisema mbegu hizo zikitumika vizuri wakulima watakuwa na uhakika wa kuvuna tani mbili hadi tatu kwa hekta moja.

Alisema Serikali bado inayo dhamira ya dhati ya kuinua zao la soya kwa kumsaidia mkulima kupata ruzuku ya pembejeo na masoko ya uhakika .

Baadhi ya wakulima wa zao hilo, walisema endapo utafiti wa mbegu hizo utafanikiwa wakulima wataongeza tija ya uzalishaji na kipata chao.

Mmoja wa wakulima hao, Tumsifu Kawaga, alisema Mkoa wa Mbeya una ardhi inayokubali zao hilo lakini wakulima wanakwepa kulima kwa hofu ya kukosa masoko.

Aliomba ujio wa mbegu hizo uendane na kuwatafutia masoko ya uhakika wa zao hilo kama ilivyo kwa maharage.



## Naibu Waziri, TIC kutatua changamoto za uwekezaji

**Na Gwamaka Alipipi**

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Stanslaus Nyongo, ameeleza nia ya wizara yake kushirikiana na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), ili kurahisisha uwekezaji pamoja na kukabiliana na changamoto zinazokwamisha shughuli hizo.

Alitoa kauli hiyo juzi alipotembelea TIC kwa mara ya kwanza tangu alipoteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan mwezi Juni 2024.

Akiwasili TIC, Nyongo alipokelewa na uongozi wa TIC chini ya Mkurugenzi Mtendaji Gilead Teri, pamoja na mambo mengine aliahidi kushirikiana kwa karibu na uongozi wa taasisi hiyo kufikia malengo ya kuimarisha uwekezaji nchini.

Aidha, alisema atashirikiana bega kwa bega na TIC kurahisisha uwekezaji na kukabiliana na changamoto zinazokwamisha shughuli za uwekezaji.

Pia aliwahakikishia TIC ushirikiano wake wa dhati, akisisitiza umuhimu wa kuondoa vikwazo vyote vinavyokwamisha uwekezaji nchini.

"Tutahakikisha tunajenga mazingira rafiki ya uwekezaji ili kuwavutia wawekezaji zaidi nchini, kwa sababu bila ya kuwa na wawekezaji uchumi wa nchi hauwezi kuendelea," alisema.

Kadhalika, uongozi wa TIC ulitumia fursa hiyo kumweleza Naibu Waziri kuhusu shughuli mbalimbali za kituo cha uwekezaji, ikiwa ni pamoja na kukuza uwekezaji katika sekta muhimu.

Taasisi hiyo pia ilielezea changamoto kadhaa inazokabiliana nazo katika kutekeleza majukumu yake na kurahisisha uwekezaji nchini, huku ikisisitiza umuhimu wa msaada wa serikali ili kuongeza ufanisi wake.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa TIC, Gilead Teri, alimweleza Nyongo jinsi TIC inavyosaidia na kurahisisha uwekezaji nchini, pamoja na majukumu yake kwa ujumla.

Pia alimweleza kuhusu huduma ya usajili wa kampuni kwa wawekezaji na vivutio mbalimbali vinavyotolewa na TIC.

Baada ya kuhitimisha ziara hiyo, Naibu Waziri alionesha matumaini kuhusu mustakabali wa uwekezaji nchini Tanzania na kuahidi kufanya kazi kwa bidii ili kuhakikisha kwamba Tanzania inakuwa mahali pazuri kwa wawekezaji wa ndani na wa kimataifa.

# Rais Dk. Mwinyi: Tutabuni matamasha kuvutia watalii

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema serikali itahakikisha inaimarisha matamasha yote visiwani Zanzibar, ikiwamo la Mwaka Kogwa na kubuni mengine mapya kwa lengo la kuongeza vivutio vya utalii.

Aliyasema hayo jana katika Tamasha la Utamaduni la Mwaka Kogwa huko Makundichi Mkoa wa Kusini Unguja na kueleza kuwa hatua hiyo itasaidia kuongeza idadi ya watalii wanaoitembelea Zanzibar na kudumisha mila, utamaduni na desturi ya Mzanzibari.

Tamasha hilo la kijadi na utamaduni hufanyika kila mwaka katika kijiji hicho ambalo ni kivutio kikubwa kwa wenyeji na wageni kutoka mataifa mbalimbali duniani.

Dk. Mwinyi alisema tamasha hilo ni fursa nyingine kwa wananchi wa Mkoa wa Kusini Unguja kama ilivyo kwa tamasha la Kizimkazi, linalofanyika kila mwaka mkoani humo kwa kupata umaarufu ndani na nje ya Tanzania.

Alisema matamasha hayo huwavutia wageni kutoka sehemu mbalimbali za Tanzania pamoja na watalii kutoka nje ya nchi kusherehekea na wenyeji.

Aidha, Dk. Mwinyi aliutaka uongozi wa mkoa huo kuwa na mipango mizuri ya kuhakikisha matamasha hayo yanaleta manufaa kwa kuleta fursa mbalimbali za maendeleo zinazoambatana na matokeo hayo.

Dk. Mwinyi alisema matumaini yake tamasha hilo katika miaka ijayo kutakuwa na matokeo zaidi ya kuongeza shamrashara, kuwataka wafanyabiashara kutumia fursa ya kuwapo kwa tamasha hilo kudhamini na kutangaza huduma zao kwa wananchi na wageni wanaofika Zanzibar.

Hata hivyo, aliwataka wamiliki wa hoteli ya kitalii kutoa ushirikiano kwa serikali ya mkoa na kutumia fursa ya tamasha hilo kuleta wageni.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohamed, alisema Makunduchi ni kijiji pekee kinachoendeleza na kudumisha mila na tamaduni, hivyo serikali itahakikisha wanazilinda tamaduni zao.

Mwenyekiti wa tamasha hilo, Mwita Masemo, alimshukuru Dk. Mwinyi kwa kuchangia shilingi milioni tano kwa ajili ya sherehe hizo.



Watoto wa dini ya Kiislamu Jumuiya ya Shia, wakishiriki matembezi ya amani ya kukumbuka kifo cha Imam Hussein, yaliyofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Amani ndiyo mlango mkuu wa uchumi Z'bar'

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema amani ndiyo mlango mkuu wa uchumi wa Zanzibar.

Amesema Zanzibar ina uzuri na utajiri mwingi wa asili ambao unahitaji viongozi imara wenye uoni mkubwa wa kuheshimu misingi ya haki, uwajibikaji na utawala wa sheria.

Aliyasema hayo ofisini kwake Migombani visiwani hapa alipofanya mazungumzo na ujumbe maalum wa Baraza la Wawakilishi la Marekani.

Othman alisema Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) siyo suluhisho pekee la kudumu la matatizo ya kisiasa ya Zanzibar, bali kunapaswa kuwapo kwa siasa safi na demokrasia ya kweli ambayo itategemea utawala bora, uwajibikaji na kuheshimu haki za binadamu.

Alisema kuwa amani ndiyo mlango mkuu wa uchumi na Zanzibar, ambayo ina uzuri na utajiri mwingi wa asili ambao unahitaji viongozi imara wenye uoni mkubwa wa kuheshimu misingi ya haki, uwajibikaji na utawala wa sheria.

Alisema hali hiyo itasababisha kuikuza nchi katika maendeleleo, huku akitolea mfano nchi ya Mauritius ambayo ni ndogo kijiografia na iliyochelewa kupata uhuru lakini wameweza kujiimarisha kiuchumi kupitia demokrasia ya kweli na hatimaye kujitegemea.

Alisema imani ya wananchi kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025, inaweza kurudi baada ya kutoweka iwapo haki zao zitaheshimiwa hususani mazingira ya sasa ambapo wengi wao mamlaka zimewanyima hata vitambulisho vya ukazi pamoja na kushiriki kujiandikisha kwa ajili ya kupiga kura, mambo ambayo kwa mujibu wa Katiba kila mtu anastahiki.

Aidha, alisema wajibu wa kuwa na Tume Huru ya Uchaguzi ambayo itaheshimu maamuzi ya wananchi walio wengi katika kujenga uongozi wa nchi uliowekwa kwa ridhaa na misingi ya demokrasia.

Othman alisema dhamira ya Serikali ya Zanzibar katika kukabiliana na athari za mazingira zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi, kasi ya ongezeko la idadi ya watu, ukosefu wa ajira, sambamba na kuimarisha sekta za utalii, gesi na mafuta na uchumi wa bluu.

Pia alitilia mkazo uwepo wa mshikamano katika kuwaendeleza wanawake kiuchumi na kusaidiana kuimarisha sekta mbalimbali zikiwamo za mazingira, afya, killimo, ukuzaji wa ajira, uvuvi, pamoja na kujenga uwezo wa wananchi kufaidika na mazao ya baharini.

Mwakilishi kutoka Chama cha Democratic katika Baraza la Wawakilishi Marekani, Katherine Clark, alisema kukutana na Makamu wa Rais siyo tu wamejifunza mambo muhimu, bali pia wamevuna mengi yenye maana, huku akisisitiza kuwa Marekani itaendeleza uhusiano mzuri uliopo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**ALVICE BAZIL MUSHI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA PASSPORT NO, **TAE 047190** ILIYOTOLEWA NA OFISI YA UHAMIAJI 20 AUG 2018 DAR ES SALAAM. YEYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA: **PHQ/ KIL/MOS/RB/16431/2023**

## KUPOTEA KWA KIBALI

**TUMAINI WILFRED KERETH** Anatangaza kupotelewa na kibali cha kuendesha BUREAU chenye namba za usajili **BCL.0596-00 .** Kwa atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi: **PHQ/ARU/ARU/25147/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RICHARD FANUEL MOLLEL** anatangaza kupotea kwa akadi ya gari yenye namba za usajili **T 160 AWT MISTUBISHI PAJERO,** kwa atakayeiona atoe taatifa kituo cha polisi **PHQ/ARU/ARU/23547/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**EMMANUEL PATRICK LUVINGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 449 DYC.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/IRI/IRI/10447/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA GARI

**YADON MTARIMA KOHI** anatangaza kupotea kwa kadi za gari zenye usajili namba **T 790 APM na T 500 CJZ .** kwa yeyote atakaezionа atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**PHQ/DAR/KIN/147112/2024**
**PHQ/DAR/KIN/147108/2024**

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA KINONDONI MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 205 LA 2024**

**TUJIJENGE TANZANIA LIMITED**
**MBOGO AUCTION MULTI AND REAL AGENCY LIMITED**
**SAHOZA AUCTION MART ........WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

**JUMA POLI**
**YOTHAM WILLIAM YUIVIGWA...WADAIWA**
**HAWA MHINA**
**RASHID MHINA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

**JUMA POLI**
**YOTHAM WILLIAM YUIVIGWA**

**POPOTE/MLIPO**

**TUJIJENGE TANZANIA LTD & OTHERS** wamefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala) . Shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 18/07/2024 saa 3:00 Asubuhi mbele ya **Mh. R.L. CHENYA** Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 11 mwezi 07…, 2024

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**INNOCENT JOSEPH URASSA** anatangaza kupotea kwa kadi ya bajaji yenye usajili namba **MC 500 CFW,** CHASSIS NAMBA: **MD2A25BY7JWH** na ENGINE NAMBA: **AZZWJH3386.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**PHQ/DOD/DOD/29910/2024**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA FOR DODOMA AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 11502/ 2024**

**In the matter of the Estate of the late ALFPHONCE NTINDA**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION PROBATE BY AGNES LUSAMBO**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Probate Rules Gn 369 of 163)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 15 Day of AUGUST, 2024

Date at Dodoma this 21 Day of APRIL, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA JUDICIARY**

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA (MOROGORO SUB-REGISTRY) AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTARATION**

**CAUSE NO 14229 OF 2024**

**In the Matter of the Estate of the Late Pius Jeremia Mbwilo**

**By James Pius Mbwilo.**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above - named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the day of 31st day of July 2024.
Dated at Morogoro this 12th day of July 2024.

DEPUTY REGISTRAR

---

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710. E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***
***Tupigie: +255 - 0677 020701***

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Marekani, Iran zalaumiana jaribio la kumuua Trump

**WASHINGTON,** MAREKANI

MATAIFA ya Marekani na Iran yameingia katika majibizano makali kuhusu tukio la jaribio la kumuua mgombea wa urais, Donald Trump.

Juzi maofisa wa usalama wa Marekani walisema kuwa ulinzi uliimarishwa wiki kadhaa zilizopita baada ya kugundulika njama zilizofanywa na Iran ya kumuua kiongozi huyo wa zamani.

Hata hivyo, Iran haikuchelewa kutoa taarifa ya kupinga taarifa hiyo ikidai ni njama ya kutumika katika kampeni ya uchaguzi wa nchi hiyo utakaofanyika Novemba mwaka huu.

Maofisa hao walisema hakuna uhusiano unaojulikana kati ya madai ya njama hiyo ya Iran na jaribio la kumuua mgombea huyo wa Republican siku ya Jumamosi wakati akihutubia wafuasi wake katika eneo la Pennsylvania.

Licha ya taarifa hiyo, bado kuna maswali zaidi kuhusu mtu aliyetekeleza jaribio hilo, Thomas Matthew Crooks (20), alivyoweza kupanda jengo na kukaribia eneo la mkutano na kisha kumfyatulia risasi Trump.

Kulingana maofisa hao, Idara ya Huduma ya Siri ya Marekani na kampeni ya Trump zilitaarifiwa kuhusu tishio hilo kutoka Iran, na hivyo usalama uliimarishwa.

Vyanzo vya kijasusi viliambia kituo cha habari cha CBS, kwamba huduma ya siri iliimarisha usalama mwezi Juni ili kukabiliana na tishio hilo.

Hatua hiyo ilijumuisha ofisa wa ziada wa kukabiliana na mashambulizi na mpiga risasi kwa kuvamia, ndege zisizo na rubani na mbwa wa roboti.

CBS iliripoti kwamba maelezo ya uwezekano wa operesheni ya Iran yalipatikana kupitia intelijensia ya chanzo cha kibinadamu, huku kukiwa na ongezeko kubwa la mazungumzo nchi hiyo kuhusika mashambulizi dhidi ya Trump.

Trump na maofisa akiwamo waziri wake wa zamani wa mambo ya nje, Mike Pompeo, walipata vitisho kutoka Iran tangu mwaka 2020 baada ya kuamuru kuuawa kupitia ndege isiyo na rubani kwa Qassim Soleimani, ambaye alikuwa kamanda wa kikosi cha Quds.

Hata hivyo, mjumbe wa Iran katika Umoja wa Mataifa, uliita madai hayo hayana uthibitisho na yenye nia mbaya.

Aliongeza kwamba Trump ni mhalifu ambaye lazima ashtakiwe na kuadhibiwa katika mahakama ya sheria.

Baada ya taarifa hiyo ya Iran kutolewa, msemaji wa Huduma ya Siri ya Marekani, Anthony Guglielmi, alisema shirika hilo na mengine usalama yamekuwa yakipokea taarifa mpya za vitisho na kuchukua hatua kama inavyohitajika.

"Hatuwezi kutoa maoni juu ya vitisho vyovyote, zaidi ya kusema kwamba huduma ya siri inachukukulia vitisho kwa uzito na kujibu ipasavyo." Alisema.

Aidha, kamati ya kampeni ya Trump ilisema haitoi maoni yoyote katika suala la usalama na ilielekeza maswali yote yaelekezwe Idara ya Huduma ya Siri.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje Iran, Nasser Kanani, alieleza katika taarifa yake kuwa nchi yake inapuuza kuhusu madai ya kuhusika katika shambulio dhidi ya Trump, na kusisitiza madai hayo yana malengo ya kisiasa.

"Hata hivyo, uchunguzi wa jaribio la mauaji ya mgombea wa Chama cha Republican haujabaini uhusiano wowote kati ya mshambuliaji na washirika wanaowezekana kuwa ni watu wa kigeni au wa ndani," alisema msemaji wa Baraza la Usalama la Kitaifa la Marekani, Adrienne Watson.

*BBC*



Wakazi wa Kijiji cha Kinsele, karibu na mji wa Goma nchini DRC wakiwa katika hali ya majonzi na hofu baada ya wanamgambo kufanya shambulizi katika eneo hilo na kuua watu 72. **PICHA: AP PHOTO**

# Israel yazidi kuichapa Gaza

**GAZA,** PALESTINA

MAMLAKA ya Ukanda wa Gaza, unaoongozwa na Hamas, umesema Wapalestina 44 wameuawa katika mashambulizi matatu tofauti yaliyofanywa na Jeshi la Israel jana.

Msemaji wa Shirika la Ulinzi wa kiraia wa Gaza, Mahmud Bassal, alisema mashambulizi hayo ya anga yamesababisha vifo hivyo na kujeruhi wengine kadhaa ndani ya saa moja.

Hata hivyo Israel ilithibitisha kufanya mashambulizi mawili.

Wizara ya Afya ya Gaza imeripoti shambulizi lililolenga kituo cha mafuta, katika eneo la Al-Mawasi kusini mwa Gaza na kuwaua watu 17, na lingine katika Shule ya Al-Razi inayosimamiwa na Umoja wa Mataifa katika kambi ya wakimbizi ya Nuseirat katikati mwa Gaza na kusababisha vifo vya watu watano.

Hata hivyo, Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu aliapa kuongeza shinikizo kwa Hamas.

"Huu ndio wakati mahsusi wa kuongeza shinikizo zaidi, kuwarudisha nyumbani mateka wote, waliohai na waliokufa na kufikia malengo yote ya vita. Wako chini ya shinikizo linaloongezeka kwa sababu tunawaumiza, kuwaondoa makamanda wao wakuu na maelfu ya magaidi. Wako chini ya shinikizo kwa sababu tunabaki thabiti katika malengo yetu," alisema Netanyau.

# Ford yakana kufadhili maandamano Kenya

**NAIROBI,** KENYA

SHIRIKA la Ford Foundation lenye makao yake nchini Marekani, limekanusha madai ya Rais William Ruto kwamba linafadhili maandamano ya kupinga serikali.

Katika taarifa walioitoa kwenye mtandao, taasisi hiyo ilimesema, Ingawa inatambua haki ya Wakenya kutetea kwa amani kuwa na nchi yenye haki na usawa, lakini haihusiki na vitendo au matamshi yoyote ambayo yana chuki au kuunga mkono unyanyasaji dhidi ya taasisi yoyote, mtu binafsi au jamii yoyote.

"Hatukufadhili maandamano ya hivi majuzi dhidi ya muswada wa fedha na tuna sera isiyopendelea upande wowote kwa utoaji wetu wote wa ruzuku." Ilisema taarifa hiyo.

Hayo yanajiri baada ya Rais Ruto kulitaja shirika hilo kuwa linafadhili maandamano na kuwaambia Wakenya kwamba kweli linahusika.

Rais Ruto aliongeza kuwa wote wanaohusika watakabiliwa na mkono wa sheria.

Shirika la Ford ni taasisi ya kibinafsi lililoanzishwa mwaka 1963 na Edsel Ford, ambaye ni mtoto wa mwanzilishi wa Kampuni ya Ford Motor, Henry Ford.

Shirika hilo linalenga kuendeleza haki na maadili ya demokrasia na kuendesha shughuli zake duniani kote.

Wakati huo huo, Tume ya kitaifa ya haki za binadamu nchini humo, ilisema idadi ya watu waliokufa kutokana na maandamano yaliyoanza mwezi uliopita imefikia 50 baada ya hapo juzi kuuawa watu wawili.

Maandamano hayo yaliyochukua siku nzima, polisi walitumia mabomu ya machozi kuwasabaratisha waandamanaji waliokusanyika katikati ya jiji la Nairobi.

Shughuli nyingi kama vile usafiri zilikwama huku maduka na ofisi za serikali zilifungwa.

Maandamano hayo yalianza mwezi mmoja uliopita yakiongozwa na vijana maarufu kwa jina la Gen Z, na kusababisha Rais Ruto kuachana na muswada wa fedha na hata kulifuta Baraza la Mawaziri.

*BBC*

## Kocha JKU atoa sababu kuvurunda Kagame Cup

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KUSHINDWA kufanya vizuri katika michuano ya Cecafa Kagame Cup, kumetokana na kukosa muda wa kujiandaa kwa kuwa msimu wa Kalenda ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), upande wa Ligi Kuu ilichelewa kumalizika, kwa mujibu wa timu ya JKU, iliyoondoshwa kwenye mashindano hayo.

Katika michezo mitatu liyocheza JKU kwenye michuano hiyo, ilishinda mmoja pekee na kupoteza miwili.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Salum Ali Haji, alisema karibu timu zote ambazo zimeshiriki michuano hiyo, ligi zao zilimalizika mapema na kupata muda mkubwa wa kufanya maandalizi ya kuelekea michuano hiyo.

Kocha huyo aliitaka ZFF kuhakikisha kalenda yao ya mashindano iangalie na kalenda ya michuano mingine ambayo timu za Zanzibar zinashiriki ili kutoa muda kwa timu zao kufanya maandalizi mazuri.

"Kalenda yetu bado haipo sawa hasa katika kuangalia mashindano mengine ambayo tunashiriki, ukiangalia tumemaliza ligi, tumepata muda mchache wa kupumzika na kurudi uwanjani, lakini ratiba yetu ya ligi kama ilivyokuwa," alisema.

Aidha, akizungumzia ushiriki wa mashindano hayo, alisema yamewapa mwanga kuelekea maandalizi yao ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Alisema wachezaji wake wamejifunza mbinu mpya, lakini pia uzoefu kwa kukutana na timu kutoka nje ya Zanzibar.

# BAJETI YA PAMBA BILIONI 1.5/-, MWINJILISTI WA KENYA AICHANGIA

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

KUELEKEA msimu mpya wa Ligi Kuu Bara Klabu ya Pamba inatarajia kutumia zaidi Sh. bilioni 1.5 kwa msimu huu huku ikiwa tayari imeshatumia takriban Sh. milioni 300 kwa usajili wa kikosi chao, imeelezwa.

Hayo yalibainishwa na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda, wakati akipokea msaada wa Sh. milioni 10 kutoka kwa Mwinjilisti Ezekiel Odero wa Kanisa la Newlife Prayer Center kutoka Mombasa Kenya, kwa ajili ya kuisaidia timu hiyo itakayouwakilisha Mkoa wa Mwanza kwenye Ligi Kuu Bara msimu ujao.

Mwinjilisti huyo, aliwiwa kuisaidia Pamba FC ili kurejesha furaha kwa wakazi wa Mwanza iliyopotea takriban miaka 23 baada ya timu hiyo kushuka daraja huku akitoa ahadi ya kununua mipira mitatu, jezi jozi mbili kwa kila mchezaji wa timu hiyo.

Akizungumza baada ya kukagua Uwanja wa CCM Kirumba ambao atautumia kufanya mkutano mkubwa wa injili Julai 24 hadi 28, mwaka huu, mwinjilisti huyo alisema amewiwa kuwawezesha vijana hao ili waweze kufikia malengo yao ya kisoka na kurejesha furaha kwa wananchi wa Mwanza.

"Ninaomba kama kunaweza kupatikana duka zuri linalouza 'unifomu' (jezi), kati ya leo (jana) na wiki ijayo, tunaweza kupanga na kuzilipia pea (jozi) mbili na mipira mitatu ambayo itasaidia timu kucheza vizuri. Timu inahitaji jezi nzuri zilizodizainiwa vema zikiwa na majina ya wachezaji," alisema Ezekiel.

Aliongeza kuwa Mwenyezi Mungu akiwapa neema baada ya mkutano watapita kuwasalimia wachezaji na watachangia kile ambacho Mungu amewawezesha kwa sababu Mungu huweka watu uongozini kwa ajili ya wale wanaoongozwa waishi maisha mazuri kama wale walio uongozini hivyo neema ambayo watajaliwa itawasaidia na wao pia.

"Mimi kipindi cha nyuma nilikuwa mchezaji na nilicheza namba 11, lakini kwa sasa siwezi tena kucheza, lakini naweza kuwawezesha vijana na kuwashika mkono," alisema.

Kwa upande wa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mtanda alisema moja ya kilio cha wananchi ni kuona timu yao inasimamiwa vema ili iweze kufanya vizuri katika michuano ya Ligi Kuu, hivyo wametumia takriban Sh. milioni 300 kwenye usajili kuhakikisha wanakuwa na timu bora.

Alisema mwezi wa nane watafanya tamasha kubwa ili kufanikisha ununuzi wa basi ambalo linagharimu Sh. milioni 450 ambapo wao wameshakusanya milioni 250 na wanaendelea kuwahamasisha wadau mbalimbali ili waweze kuwashika mkono na wamewaomba baadhi ya viongozi wizarani wasaidie kufanya hamasa kwa wadau ili kufanikisha ununuzi wa basi hilo.

"Na sisi tunaendelea kuhamasisha, tumepata wadau ambao wametudhamini takriban Sh. milioni 400 za uendeshaji wa timu, kwa hiyo jumla kuu ya uendeshaji wa timu ni zaidi ya Sh. bilioni 1.5 kwa msimu kwa mchango huu naamini utafungua njia kwa wadau wengine kwa sababu uendeshaji wa timu ni gharama kubwa," alisema Mtanda.



Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi (kulia), msaidizi wake, Moussa N'Daw, pamoja na rais wa klabu hiyo, Injinia Hersi Said (katikati), wakifuatilia mazoezi ya timu hiyo, Kigamboni, Dar es Salaam. **PICHA: YANGA**

# YANGA WAIFUATA SIMBA UWANJA WA KMC

**Na Romana Mallya**

BAADA ya awali kuelezwa Simba ilikuwa timu ya kwanza kuomba kuutumia Uwanja wa Manispaa ya Kindononi (KMC Studium), hatimaye mabingwa wa Ligi Kuu Bara, Yanga nao wameomba kutumia dimba hilo kuelekea msimu mpya wa 2024/25, imeelezwa.

Timu hizo zimefikia hatua hiyo kutokana na msimu mpya unaotarajiwa kuanza Agosti 16, mwaka huu, hazitaruhusiwa kuutumia Uwanja wa Benjamin Mkapa kutokana na kuwa kwenye ukarabati mkubwa kwa ajili ya fainali za AFCON 2027, ambapo Tanzania itakuwa mwenyeji kwa ushirikiano wa Kenya na Uganda

Katibu wa NEC, Itikadi, Uenezi na Mafunzo CCM Taifa, Amos Makalla, amesema timu kubwa za mpira wa miguu Tanzania zimetuma maombi yao kuomba kutumia Uwanja wa Manispaa ya Kindononi, KMC Studium ambao ujenzi wake umefikia asilimia 95.

Akizungumza jana baada ya kutembelea mradi huo kuona maendeleo yake ikiwa ni sehemu ya ziara yake mkoani Dar es Salaam, kiongozi huyo alisema ameridhishwa nao.

Alisema uwanja huo umeweka historia Dar es Salaam kwa kuwa zipo timu nyingi, lakini zenye uhakika wa uwanja ni Azam na KMC.

"Kuna timu nyingine ina uwanja mzuri wa mazoezi Bunju na wengine wanapanga na kukodi. Niwaombe zile timu kubwa wale wa Bunju watengeneze uwanja kama huu na wale kule wa Kigamboni watengeneze kulinda heshima za timu zao kubwa.

"Azam na KMC wamewatangulia. Nilichofurahi hizo timu kubwa zote zinaleta maombi hapa muwapokee. Nasikia Yanga wameomba na Simba wameomba wote muwapokee ili sisi wakazi wa Dar es Salaam na mikoa ya jirani tuone mpira kutokea hapa Mwenge," alisema.

Makalla alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuruhusu fedha zitumike kujenga uwanja wa huo wa KMC.

Alisema kuna uhaba wa viwanja ambapo timu za Ligi Kuu zinapokuja huangaika na kuwaeleza kuwa wakiwa na hosteli hapo timu zitakwenda zaidi.

Mhandisi Frank Joseph, alisema uwanja huo una majukwaa ya kawaida yenye uwezo wa kuchukua watu 6,000 na umewekwa nyasi bandia.

Katika uwanja huo kwa sasa ligi inayoendelea kucheza hapo ni Dar Port Kagame Cup.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**UNITED HAIMTAKI SOUTHGATE**
KLABU ya Manchester United haina mpango wa kumchukua kocha wa zamani wa Timu ya Taifa ya England, Gareth Southgate, endapo wataamua kumfuta kazi Erik ten Hag. ***(Mail)***

**CHELSEA KUMTOA LUKAKU**
CHELSEA iko tayari kuwatoa mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 31, na kiungo wa kati wa Italia, Cesare Casadei mwenye umri wa miaka 21 kwa Napoli ili kusaidia kupunguza bei ya mshambuliaji wa Nigeria, Victor Osimhen, 25. ***(Teamtalk)***

**ARSENAL NA CALAFIORI**
ARSENAL bado haljafikia bei ya Bologna ya pauni milioni 42.3 kwa ajili ya kumnunua mlinzi wa Italia, Riccardo Calafiori mwenye umri wa miaka 22, na mazungumzo kati ya klabu hizo mbili yanaendelea. (***Football Italia***)

**ROYAL ATAKIWA MILAN**
AC Milan imetoa ofa ya awali kwa beki wa kulia wa Tottenham Hotspur na Brazil, Emerson Royal, lakini kuna pengo kati ya tathmini ya klabu kuhusu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25. ***(Sky Sports Italia)***

**GROSS HUYOOO DORTMUND**
KIUNGO wa kati wa Ujerumani, Pascal Gross, amekubali maslahi binafsi na Borussia Dortmund, ambao wako kwenye mazungumzo ya kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, kutoka Brighton kwa kati ya pauni milioni sita. (***Sky Sports Germany)***

**GALLAGHER ATAKIWA SPURS**
KLABU ya Tottenham Hotspur imehusishwa na kiungo wa kati wa Chelsea, Conor Gallagher mwenye umri wa miaka 24, lakini mchezaji huyo wa Kimataifa wa England hana uwezekano wa kuhamia Spurs msimu huu wa majira ya joto. ***(Football Insider)***

**ALMIRON SASA KUUZWA**
WINGA wa Newcastle United, Miguel Almiron yuko kwenye mazungumzo na mwakilishi wake kuhusu mustakabali wake huku mchezaji huyo wa Kimataifa wa Paraguay mwenye umri wa miaka 30, akihusishwa na kuhamia Saudi Arabia na 'Magpies' hao wanaaminika kuwa tayari kumuuza. ***(Chronicle)***

**MORATA AAMUA KUONDOKA**
MSHAMBULIAJI wa Hispania, Alvaro Morata, anatafakari iwapo ataondoka Atletico Madrid na kujiunga na AC Milan, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, akisema tayari ameamua. ***(Corriere dello Sport)***

**WIRTZ AZIDI KUGOMBEWA**
REAL Madrid ina imani kuwa inaweza kuwashinda wapinzani wao, Barcelona katika kumsajili kiungo wa kati wa Bayer Leverkusen na Ujerumani, Florian Wirtz, 21. ***(Sport)***

**MARTINEZ NA MAN UTD**
WAKALA wa mlinda mlango wa Argentina, Emiliano Martinez mwenye umri wa miaka 31, amesema Manchester United ilikuwa karibu kumsajili kutoka Aston Villa msimu uliopita wa majira ya joto, lakini kocha Erik ten Hag, aliamua kumnunua Andre Onana wa Cameroon mwenye umri wa miaka 28 badala yake. ***(ESPN)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ALVAREZ KUMRITHI MORATA ATLETICO

Kuhusu anaye mrithi kutua Milan, alisema ni lazima afaulu kwanza vipimo vya afya, lakini hilo ndilo wazo lake...

**MADRID, Hispania**

MSHAMBULIAJI wa Manchester City, Julian Alvarez, ndiye chaguo la kwanza la Atletico Madrid kuchukua nafasi ya Alvaro Morata na nahodha wa Hispania anayetarajiwa kujiunga na AC Milan msimu huu wa majira ya joto, vyanzo kwa mujibu wa ESPN.

Alvarez mwenye umri wa miaka 24, amefunga mabao 36 katika michezo 103 tangu ajiunge na mabingwa hao wa Ligi Kuu England msimu wa majira ya joto wa 2022 kutoka River Plate, lakini ameshindwa kuingia kwenye kikosi cha kwanza kwa sababu ya uwapo wa Erling Haaland.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia la 2022 akiwa na Argentina na bingwa mpya wa Copa America, Alvarez hivi majuzi alihojiwa kuhusu mustakabali wake na ingawa alisisitiza kuwa ana furaha City, aliongeza pia: "Tutaona."

Vyanzo viliiambia ESPN kwamba Atletico wanafahamu kuwa City haitawafanyia mambo rahisi kwa hivyo hawaondoi mkataba wa mkopo.

Alvarez anataka muda zaidi wa kucheza na Atletico wana furaha kumfanya kuwa mmoja wa nguzo za mradi mpya wa kocha Diego Simeone.

Kama ESPN ilivyoripoti, Atletico wamezingatia njia mbadala za kuimarisha safu yao ya ushambuliaji baada ya klabu hiyo kutangaza kuondoka kwa mshambuliaji wa Uholanzi, Memphis Depay.

Artem Dovbyk wa Girona na Alexander Sørloth wa Villarreal ni miongoni mwa wachezaji ambao 'Rojiblancos' hao imewafuatilia katika miezi ya hivi karibuni.

Lakini vyanzo viliiambia ESPN kwamba Atletico iko tayari kufanya juhudi za kifedha kumsajiki Alvarez ikiwa Morata ataondoka kwenye klabu hiyo msimu huu wa majira ya joto. Vyanzo vingine vimeithibitishia ESPN kwamba Morata tayari amekubaliana maslahi binafsi na Milan, lakini bado hajasaini rasmi.

Mustakabali wa Morata katika Klabu ya Atletico umekuwa shakani katika wiki za hivi karibuni kutokana na ripoti kwamba mshambuliaji huyo wa zamani wa Chelsea alikuwa karibu kujiunga na Klabu ya Al Qadsiah inayoshiriki Ligi ya Saudia.

Morata mwenye umri wa miaka 31, alikataa ofa hiyo na kutangaza mapenzi yake kwa Atletico kwenye mitandao ya kijamii.

Lakini vyanzo vimeiambia ESPN kwamba Morata sasa ameamua kuondoka na kuendelea na kazi yake huko AC Milan.

Mshindi huyo wa Euro akiwa na Hispania alifikia hadi kusimama mazoezi ya Atletico Madrid Jumanne na kuwaaga wachezaji wenzake.

"Ilikuwa muhimu kwangu kuja hapa na kuwaaga, kuwashukuru kwa kila kitu," Morata alisema kwenye redio ya Hispania Cope baada ya ziara hiyo.

"Daima wamenisaidia sana katika nyakati ngumu. Unapokuwa katika hali ambayo huwezi kufanya vizuri, chaguo jingine ni bora zaidi. Kwangu, katika kushinda taji la Euro niliiwakilisha Atletico na nina thamani sawa na kushinda na klabu ninayoshiriki."

Alipobanwa iwapo anaondoka au la na kujiunga na Milan, Morata alisema: "Bado ni lazima nifaulu vipimo vya afya, lakini ndio, hilo ndilo wazo."

# FLICK AMTAKA OLMO BARCELONA SI WILLIAMS

**BARCELONA,** HISPANIA

BARCELONA inaonekana kumfanya Nico Williams kuwa mlengwa wao mkuu msimu huu, baada ya kiwango chake cha kuvutia kwenye Euro 2024, lakini kocha Hansi Flick anaripotiwa kumtaja Dani Olmo.

Inaonekana Barcelona wataweka kila walicho nacho katika kumsajili Williams msimu huu wa majira ya joto, ambapo inamaanisha kukubaliana naye na kuamsha kipengele chake cha kuruhusiwa kuondoka kwa euro milioni 58 katika Klabu ya Athletic.

Sehemu ya sababu ni kwamba wanahisi ataibua msisimko miongoni mwa mashabiki.

Lakini Sport imeripoti kuwa idara ya michezo, inayojumuisha Mkurugenzi wa Michezo, Deco na kocha Flick, ingependelea kumsajili Olmo.

Nyota huyo wa RB Leipzig pia ana kipengele cha kuruhusiwa kuondoka kwa euro milioni 60, ambacho kinamalizika Jumamosi.

Lakini kulingana na kile kinachotokea na Williams, wanatumaini wataweza kufanya mazungumzo na Leipzig.

Pia wanabainisha kuwa Manchester City, licha ya kukataliwa, Bayern Munich, Liverpool na Manchester United zote zinamuwaniwa msimu huu wa majira ya joto.

Flick na Deco wangempendelea Olmo kwani wanahisi kuwa ana uwezo mwingi zaidi na mzoefu zaidi katika kikosi ambacho tayari ni kichanga.

Hakika maonesho ya Olmo kwa Hispania yalikwenda chini ya rada kwa sababu ya mlipuko wa Williams na Lamine Yamal, lakini mwishowe, neno la Laporta ni sheria huko Barcelona.



# Alexander-Arnold awaniwa Madrid

**MADRID,** HISPANIA

REAL Madrid imeripotiwa kuchukua hatua madhubuti katika harakati zao za kutaka kumsajili beki wa kulia wa Liverpool, Trent Alexander-Arnold.

Alexander-Arnold ameingia miezi 12 ya mwisho ya mkataba wake na Liverpool, huku mazungumzo ya kuongeza muda yakicheleweshwa.

90minute iliripoti kwa mara ya kwanza kuhusu nia ya Madrid kwa Alexander-Arnold Machi mwaka huu, wakati beki huyo wa kulia alijulikana kuwa na utulivu na kuelewa kuhusu kuchelewa kutatua mustakabali wake Anfield.


Hata hivyo, sasa katika mwaka wa mwisho wa mkataba wake wa sasa, hali ya Alexander-Arnold imeibua nia ya pande kadhaa za juu na inadaiwa Madrid sasa wana nia madhubuti kutaka kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25.

Inadaiwa kuwa Madrid wamekuwa wakiwasiliana na Alexander-Arnold kwa mwezi mmoja uliopita na nyota huyo wa Liverpool ameonesha nia ya kuhamia Santiago Bernabeu.

Baada ya kuhitimisha safari yake ya Euro 2024 na England, Alexander-Arnold atakuwa huru kuzungumza na Liverpool kuhusu mustakabali wake.

"Ulikuwa msimu mzuri, uliojengwa juu ya msimu uliopita, ulikuwa bora kama timu, ulishindania ubingwa, ulifika mbali na tukaimarika," alisema.

"Wakati wowote unapoimarika inamaanisha kuwa ni msimu mzuri. Chukua chanya na usonge mbele na tunatumai tena msimu ujao."



# Ufaransa yailalamikia Argentina kwa ubaguzi

**PARIS,** UFARANSA

SHIRIKISHO la Soka la Ufaransa (FFF), litawasilisha malalamiko ya kisheria juu ya "matamshi ya kibaguzi na ubaguzi" ya wachezaji wa Argentina katika nyimbo zao kuhusu Timu ya Taifa ya Ufaransa baada ya fainali ya Copa America.

Argentina iliifunga Colombia bao 1-0 Jumapili. Video iliyowekwa kwenye Instagram na kiungo wa Argentina, Enzo Fernandez na kutazamwa sana kwenye mtandao X, ilionesha wachezaji wa Argentina wakiimba kuhusu wachezaji wa Ufaransa wenye asili ya Afrika.

Baadaye Fernandez aliomba msamaha kwa kuimba wimbo ulioangaziwa kwenye video hiyo.

Nyimbo zile zile - za baadhi ya mashabiki wa Argentina - ziliibuka kabla ya Ufaransa na Argentina kukutana katika fainali ya Kombe la Dunia miaka miwili iliyopita, ambapo Argentina ilishinda.

"Kutokana na uzito wa matamshi hayo ya kushangaza ambayo ni kinyume cha maadili ya michezo na haki za binadamu, rais wa FFF ameamua kuwasiliana na mwenzake wa Argentina na FIFA moja kwa moja ili kuwasilisha malalamiko ya kisheria kwa matamshi ya kibaguzi na ubaguzi," shirikisho la Ufaransa lilisema. katika taarifa yake.

"Rais wa Shirikisho la Soka la Ufaransa, Philippe Diallo, analaani vikali matamshi yasiyokubalika ya kibaguzi dhidi ya wachezaji wa wa Ufaransa kama sehemu ya wimbo ulioimbwa na wachezaji na wafuasi wa Timu ya Taifa ya Argentina."



HABARI MICHEZO

# YANGA KINARA MASHABIKI WENGI UWANJANI, SIMBA MAPATO ZAIDI

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imeongoza kwa kuingiza mashabiki wengi kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita, huku watani zao wa jadi, Simba wao wakiwa vinara wa mapato viwanjani kwa msimu wa 2023/24.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotokea jana na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), JKT Tanzania ndiyo timu iliyopata mapato kiduchu zaidi, huku Mtibwa Sugar iliyoshuka daraja, ikiingiza mashabiki wachache zaidi kati ya timu zote 16 zilizoshiriki Ligi Kuu msimu uliopita.

Takwimu zinaonyesha kuwa Yanga imeongoza, ikiingiza jumla ya mashabiki 141,911 kwa msimu, ikifuatiwa na Simba ambayo iliingiza mashabiki 112, 717.

Timu ya Mashujaa FC, yenye maskani yake mjini Kigoma, imeshika nafasi ya tatu, ikiingiza mashabiki 45,638, huku Tabora United ikiwa nafasi ya nne, ikikusanya 43,808 na Azam FC, imekuwa ya tano ikiingiza jumla ya mashabiki 35,379.

Kwa mujibu wa takwimu hizo za TFF, nafasi ya sita imechukuliwa na Dodoma Jiji, yenyewe ikiwa na mashabiki 30,381, Geita Gold ambayo imeshuka daraja, ikiwa ya saba, ikiingiza 24,774, Coastal Union ikikamata nafasi ya nane, mashabiki wake ni 24,161, maafande wa Prisons wakiwa kwenye nafasi ya tisa, wakiwa na mashabiki 24,147, na nafasi ya 10 imeenda kwa Singida Fountain Gate, ambayo kwa msimu mzima imeingiza mashabiki 21,154.

Mtibwa Sugar ni ya mwisho, ikiingiza mashabiki 7,529, ambayo ndiyo walioingia Uwanja wa Manungu Complex, kutazama mechi za Ligi Kuu msimu uliopita.

Simba imeingiza kiasi cha Sh. 835,805,000 na kuwa kinara wa mapato kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliomalizika, ikifuatiwa na Yanga ambayo imeingiza Sh. 825,065,000 kwa msimu mzima wa ligi hiyo.

Tabora United imekamata nafasi ya tatu kwa wingi wa mapato, ikikusanya Sh. 223,270,000, wakati Mashujaa FC, ikiwa nafasi ya nne, ikiingiza Sh. 140,702, 000.

Singida United, iko nafasi ya tano, yenyewe ikiingiza Sh. 135, 045,000 na namba sita inashikiliwa na Dodoma Jiji ambayo imekusanya Sh. 126,722,000, Geita Gold ambayo imeteremka daraja, ikivuna Sh. 119,046,000 na imeshika nafasi ya saba, Prisons iko nafasi ya nane na Sh. 118, 835,000 zake, wakati Azam FC imekamata nafasi ya tisa, ikiingiza kiasi cha Sh. 116,048,000 na nafasi ya kumi imetwaliwa na Costal Union, ikiingiza Sh. 102, 509,000.

Timu ya JKT Tanzania imepata pesa kiduchu msimu uliopita, ikiambuliwa Sh. 32,054,000 za mapato yao yote ya mlangoni.

## Kanuni Fifa zaibeba Simba SC kwa Lawi

INATOKA UK. 24

kuwa bado inaendelea, wakati wanasainiana ilikubaliwa ligi ikiisha wampeleke kufanyiwa vipimo, malalamiko yao ni kwamba Simba walichelewesha malipo zaidi ya tarehe hiyo, yalifanyika Juni 10.

"Simba wao walisema walichelewa kwa sababu walikuwa wanasubiri wamfanyie vipimo, ikiwa ni moja kati ya matekelezo ya kimkataba, haikuwezekana kwa sababu aliitwa kwenye kikosi cha Taifa Stars, lakini baadaye Simba walilipa bila hilo kutekelezeka," alisema na kuongeza;

"Ushahidi unaonyesha kuwa mpaka Juni 3, Simba na Coastal walikuwa wanaendelea na mazungumzo. Ilipolipwa, tarehe 17, wakaandika barua ya kusitisha mkataba ikiwa ni siku 10 baada ya kupokea pesa yote."

Akabainisha Coastal hawakufanya vyote hivyo ambavyo walitakiwa kuvifanya, na hata kama ingekuwa vinginevyo, walipaswa kupeleka shauri TFF kwenye kamati husika na si kumzuia mchezaji na kudai kuvunja mkataba, kitu ambacho hawana mamlaka nacho.

Wakati hayo yakiendelea, Mwenyekiti wa klabu hiyo, Steven Mguto, ametishia kuishtaki Klabu ya Simba hata kama maamuzi yatakuwa upande wao.

Alisema endapo wangefuata makubaliano hayo, swala hilo lisingefika lilipo sasa na akazitaka klabu zingine kuwa makini kipindi hiki cha usajili ili kujiepusha na usumbufu kama huo.

"Tunasubiri maamuzi yatolewe, tukiwa tumeshinda lazima tuishitaki kwa kosa la kumtangaza mchezaji wetu huku wakiwa hawakutimiza makubaliano tuliyokubaliana, alisema Mguto.

Wakati huo huo, Klabu ya Simba imemtambulisha kiungo mshambuliaji, Awesu Awesu, aliyesajiliwa kutoka KMC.

Mchezaji huyo amewahi kuzichezea klabu mbalimbali nchini kwa nyakati tofauti kama, Mwadui FC, Kagera Sugar, Azam FC, kabla ya kujiunga na KMC.

Ataungana na wenzake waliopo nchini Misri kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya wa mashindano.



## Ukarabati kwa Mkapa sasa wafikia asilimia 35

**Na Shufaa Lyimo**

UKARABATI unaoendelea katika Uwanja wa Benjamin Mkapa hadi sasa umefikia asilimia 35, huku mkandarasi akiendelea kupambana ili kukamilika kwa wakati, kwa mujibu wa serikali.

Maboresho hayo ni kwa ajili ya maandalizi fainali za AFCON 2027, ambapo Tanzania kwa kushirikiana na nchi za Kenya na Uganda, zitakuwa wenyeji wa michuano hiyo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana baada ya kupokea ujumbe kutoka Shirikisho la Soka Afrika (CAF), uliofanya ukaguzi wa uwanja huo juzi, Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa, alisema ukarabati huo unabebwa na ununuzi wa vifaa vya ujenzi kitu ambacho kinasababisha kuonekana asilimia zilizokamilika kuwa chini.

Alisema kwa sasa mchakato unaoendelea ni katika ununuzi wa viyoyozi, vifaa vya zimamoto, vifaa vya mfumo wa majisafi na majitaka, sauti, taa ambazo tayari zimefungwa nusu .

„Inawezekana leo asilimia zikawa chini kidogo sababu kubwa ni gharama za ukarabati na vifaa vipo katika mchakato na vikikamilika asilimia itaongezeka na eneo kubwa linalochukua gharama ni ufungaji wa viti vilivyopo zaidi ya 62,000 vitabadilishwa kwa asilimia 100," alisema Msigwa.

Katibu huyo alisema ujumbe huo wa CAF utakwenda pia kufanya ukaguzi kwenye Uwanja wa Arusha, Uwanja wa Amaan na Fumba wa Zanzibar ikiwamo ukaguzi viwanja vitano vya mazoezi katika maeneo hayo.

Aliongeza kuwa, tayari serikali imeshatoa fedha za kuanzia ujenzi wa Uwanja wa Arusha lengo likiwa ni kuhakikisha wanatekeleza matakwa ya CAF kwa kukamilika kwa wakati na kuwa katika utayari wa kuwa mwenyeji wa AFCON 2027.

Alibainisha kuwa matumizi ya matukio mbalimbali ya ndani na nje yamekuwa yakimkwamisha mkandarasi kumaliza kwa mujibu wa mkataba ambao unamtaka kuhakikisha ifikapo Agosti 24, mwaka huu, ukarabati huo uwe umekamiliki.

„Nipende kutumia nafasi hii kuomba wadau wanaokuja kuomba kutumia viwanja vya Benjamin na Uhuru wajipange kutafuta maeneo mengine ya kufanyia shughuli zao ili kupisha ukarabati ukamilike na hata kukwepa penalti," aliongeza.

## Yanga yawageuka rasmi kina Magoma

INATOKA UK. 24

kwao," alisema.

Hata hivyo, alisema walichogundua ni kwamba mmoja wa waliodai kuwa ni mjumbe wa Baraza la Wadhamini yupo upande wa walalamikaji.

"Tulichogundua ni kwamba iliendeshwa kwa upande mmoja, hao watu kugawana majukumu upande wa mlalamikaji na mlalamikiwa, kwa maana Juma na Mwaipopo walikaa upande wa mlalamikaji na Abeid alikaa upande wa mlalamikiwa, huku akiwawakilisha wadhamini.

"Katika shauri, Abeid, aliwasilisha utetezi wa mama Fatma uliosainiwa naye, pamoja Katundu, mlalamikiwa namba tatu, akidai wote wamemteua kuwawakilisha kwenye mwenendo wa kesi hiyo, na utetezi wa wote hao ulifanywa na yeye, hivyo alikuwa akikubali kila kitu kilichokuwa kikisemwa au kuombwa mahakamani, hivyo kusababisha hukumu ya Agosti 22, 2023 kuwapa ushindi walalamikaji kwa sababu haikuwa inapingwa," alisema.

Alisema baada ya hukumu hiyo, Mei 24, mwaka huu, walipeleka maombi ya kukazia hukumu mbele ya Hakimu Mkazi, Kisutu, ikiwamo kulitoa na kulifuta baraza la wadhamini wa Yanga na kuutoa uongozi wote, kutaka wakabidhiwe timu na mali zote za klabu ili waendeshe wao, Juni 10 klabu lilipata taarifa hiyo, hivyo uongozi ulituma jopo la mawakili akiwamo yeye kufuatilia suala hilo kwa undani.

Alisema kufuatia hayo, jopo la wanasheria limetuma maombi kuomba waongezewe muda wa kufanya mapitio ya kesi na wanaamini wataitwa kusikilizwa kwa kuwa hawakushirikishwa.

"Klabu imetuma maombi ya kupitia upya kesi hiyo kwa sababu hatukushirikishwa na walalamikaji hawakuwa na uhalali wowote, vile vile walifanya kosa la jinai kufoji sahihi za viongozi wakubwa wa klabu tunaamini mahakama itatutendea haki na inaonekana kuna watu wanaowatumia kuleta uchochezi. Tumeanza uchunguzi na ikibainika, wahusika wote watapelekwa kwenye mkutano mkuu, pili tukishaongezewa muda, klabu itaomba kufanya marejeo kwa sababu walalamikaji wote hawakuwa na uhalali.


"Tatu ni maombi ya kuzuia utekelezaji wa hii hukumu ambayo walalamikaji waliiomba kuwasaidia kuuondoa uongozi wa Yanga na kukabidhiwa timu. Na nne, tumewasiliana na Mama Fatma na Katundu ili kushirikiana na uongozi wa Yanga kufungua kesi ya jinai kwa wote walioghushi saini zao kinyume cha matakwa yao," alisema.

Wakati huo huo, kikosi cha Yanga kinatarajiwa kuondoka leo mchana kuelekea Afrika Kusini kushiriki michuano ya Kombe la Toyota.

Ikiwa huko itacheza michezo mitatu, ambapo itaanza kushuka dimbani, Julai 20 kucheza dhidi ya Augsburg ya Ujerumani, Julai 24, ikitarajiwa kucheza dhidi ya TS Galaxy ya Afrika Kusini, na Julai 28 itakipiga dhidi ya Kaizer Chiefs.

Michezo
Nipashe Alhamisi Julai 18, 2024

## Alvarez kumrithi Morata Atletico
UKURASA 21



# Yanga sasa yawageuka rasmi kina Magoma

## ●●● Yaomba muda utekelezaji wa hukumu mahakamani, huku ikipaa kwenda Sauzi...

**Na Waandishi Wetu**

KLABU ya Yanga imesema waliofungua kesi ya kikatiba dhidi ya Baraza la Wadhamini wao, si wanachama wao.

Sambamba na hilo, klabu hiyo imedai saini za baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wadhamini zimeghushiwa, hivyo inaangalia utaratibu wa kisheria wa kwenda kushtaki na ikibainika sheria ichukue mkondo wake.

Yanga pia imesema imegundua kuna baadhi ya watu wasioitakiwa mema klabu wapo nyuma ya wale waliofungua shauri ili kuung'oa uongozi madarakani.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Wakili wa klabu hiyo, Simon Patrick, alisema wamegundua kesi iliyoendeshwa dhidi ya Baraza la Wadhamini, ilikuwa ni ya upande mmoja, huku pande hiyo ikijigawa na kujifanya ipo upande wa walalamikiwa.

Alisema hayo kutokana na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es salaam kutoa amri uongozi wa Yanga, ukiongozwa na Rais Injinia Hersi Said, kuondoka madarakani kwani uwapo wao waukufuata katiba ya klabu hiyo.

Inaelezwa kuwa uamuzi huu wa mahakama umekuja baada ya kundi la wazee wachache waliowahi kuwa wazee wa klabu hiyo kipindi cha nyuma kupeleka mashtaka mahakamani likidai uwapo wao hakufuata katiba.

"Novemba 6, mwaka 2022, watu wawili waljiita wanachama wa Yanga walifungua kesi katika Mahakama ya Kisutu jijini Dar es Salaam, ambao ni Juma Ally (Magoma) aliyekuwa mlalamikaji namba moja na Geofrey Mwaipopo ambaye ni mlalamikaji namba mbili na wa tatu ni Jabir Katundu.

Walifungua dhidi ya Baraza la Wadhamini kama mlalamikiwa namba moja, mama Fatma Karume, Abeid Mohamed Abeid, ambaye ni mlalamikiwa namba tatu," alisema wakili huyo.

Alisema walichokuwa wakihitaji ni kuondoka kwa viongozi waliopo, na mali za klabu na timu wakabidhiwe wao.

"Wanasema rais wa Klabu, Injinia Hersi, Makamu wake, Arafat Haji, Kamati ya Utendaji na watendaji wote walioajiriwa kwa kigezo cha unachama, wote uwanachama wao ni batili, hivyo hawafai kuiongoza klabu, hivyo walikuwa wanaiomba mahakama ituondoe wote.

Pia kazi zote ambazo zimefanywa na viongozi hao, zitambuliwe kama ni batili, hivyo waletewe ripoti ya mapato na matumizi kwa kipindi chote na klabu ikabidhiwe

INAENDELEA UK. 23



Kipa wa Yanga, Abutwalib Mshery, akiwa mazoezini. **PICHA: YANGA**

## Kanuni Fifa zaibeba Simba SC kwa Lawi

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

WAKILI Nduruma Majembe, amefunguka shauri la Simba lililopelekwa kwenye Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji kuhusu kuvunjiwa mkataba na Coastal Union wa kumsajili beki Lameck Lawi, akisema timu hiyo haikuwa na mamlaka hayo kwani walipaswa kupelekwa Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini ambao ndiyo wenye mamlaja ya kutafsiri sheria.

Akizungumza jijini Dar es Salaam kuhusu sakata hilo ambalo lilizungumzwa juzi kwenye Ofisi za TFF, Nduruma, alisema wanaamini Coastal haikufanya sahihi, kwani wao hawana uwezo huo, bali wangelipeleka kwenye vyombo maalum na si wao kuamua kuhusu suala la mchezaji huyo.

Simba ilimsajili Lawi ambaye ni beki wa kati na ilipomtangaza tu, viongozi wa Coastal Union waliibuka na kudai kuwa klabu hiyo ilikiuka makubaliano ambayo ni ya kulipa pesa kabla ya siku ya mwisho iliyoainishwa ndani ya mkataba.

Alisema mkataba wa mpira, kuna vitu vikifanyika haviwezi kupanguka kwa mujibu wa Kanuni za CAF na Fifa, ambapo mkataba ukiingiwa utakuwa tayari umeshakamilika, na malipo yana eneo lake.

"Huu si kama mkataba wa kuuziana kuku au mbuzi ambapo usipoleta pesa kesho basi unavunjika, haipo hivyo, mikataba ya mpira wa miguu ina taratibu zake.

Kama mtu hajalipa kwa siku 30 ndipo inapokuwa tatizo, na hata hivyo ni lazima uandike notisi, na baada ya hapo siku 10 baada ya kupewa ndipo klabu inatakiwa ikamilishe malipo hizo ndizo taratibu zilivyo," alisema wakili huyo ambaye aliwahi kuisimamia kesi ya Bernald Morrison dhidi ya Klabu ya Yanga miaka kadhaa nyuma.

Alisema hoja iliyopo mezani ni Coastal kusitisha mkataba wa Lawi kuichezea Simba kama ni halali au la.

"Sidhani kwamba Coastal walilalamika kutambulishwa, ila ni kwamba pesa ya klabu ilipaswa kulipwa kufikia Mei 31, na wakati huo ligi ili

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >